

MLANGO NDANI YA MLANGO



Asanteni sana.

² Mwaweza kuketi. Hakika nayahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu kuwa hapa Jumatatu hii usiku, na kuona mkusanyiko huu mzuri wa watu walio na njaa, na kiu kwa ajili ya Mungu.

³ Ninaamini Maandiko yanasema, “Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa.” Na kama Mungu ametupa ahadi hiyo iliyobarikiwa, basi kitu pekee ambacho kingetuzuia kujazwa na kila kitu tunachoonea kiu, kingekuwa ni kwa sababu hatuamini. Tukiweza tu kuamini sasa, ya kwamba Mungu atatupa kitu kile hasa kilichotuleta hapa, sote tutaenda nyumbani usiku wa leo, tukiwa na furaha sana na kuridhika.

⁴ Nina furaha sana kwamba Yeye hutupa kila haja yetu, Yeye aliahidi atafanya hivyo. Sasa, Yeye kamwe hakuahidi ya kwamba angetupatia *matakwa* yetu, bali angetupatia *mahitaji* yetu. Ninafurahia hilo sana, kwa sababu kuna mara nyingi ambapo tunataka mambo ambayo si mazuri kwetu.

⁵ Nilikuwa tu nikiwazia jambo hilo hivi majuzi, nilipokuwa nikijaribu kunyoa kwa wembe mtupu. Na ninii yangu... Nilikuwa sio stadi sana kwake, sikuwa nimewahi kuujaribu hapo awali. Naye mvulana wangu mdogo, Joseph, alikuwa akisema, “Baba, hebu nijinyoe, pia,” umri wa miaka mitano. Nami nikawazia sasa... Naye alilia kwa sababu nisingemruhusu kushika wembe. Lakini mnaona, nilijua nisingefanya hivyo.

⁶ Na hivyo ndivyo Mungu alivyo. Wakati mwingine tunafikiri ya kwamba lazima tuwe na vitu fulani, na tungejidhuru tu navyo. Kwa hiyo, kama tutakuwa tu watiifu na wanyenyekevu, kama watoto wadogo mbele Zake, Mungu atatupa tunachohitaji.

⁷ Na kama—na kama mimi, nikiwa baba wa kimwili na wa duniani, nampenda mvulana wangu mdogo vya kutosha kutomruhusu kushika wembe mtupu, haidhuru anaulilia kiasi gani, ni zaidi sana vipi Baba yetu wa Mbinguni anavyojua, ingawa tunalilia kitu ambacho tunafikiri tunakihitaji?

⁸ Lakini Yeye alituahidi ya kwamba mambo yote yangefanya kazi pamoja kwa manufaa ya wale wanaompenda Mungu. Na, tena imeandikwa, “Hatawanyima kitu chochote chema hao waendao kwa unyofu mbele Zake.” Hiyo si ni ahadi?

⁹ Kwa hiyo, daima nimekuwa na msemu mdogo ambao sikuzote nawapa watu ni: Fanya mambo matatu maishani. Jambo la kwanza ni kutenda haki, huo ni wajibu wako kwa Mungu; wazia mema, hilo ni jukumu lako kwako mwenyewe; nawe huna budi kutokea vema. Hiyo ni kweli kabisa. Wewe fanya haki, kisha

uwazie mema, na mradi tu unaenda vema, huwezi kuwa unaenda vibaya.

¹⁰ Wakati mvulana wangu, Billy, kwenye umri wa yapata miaka kumi na minne, kabla sijampeleka kwenye shule ya Biblia, alikuwa katika shule ya kawaida, wala hakuwa na msingi mzuri sana, huku watoto wote, wasichana, wavulana wakivuta sigara na kufanya vituko. Ndipo siku moja nikaingia nyumbani na kuketi chini, naye Billy alikuwa anakaa na nyanya yake, basi Uwepo wa Bwana ulipokaribia, ono lilitokea, nikamwona mvulana wangu akiwa na sigara mkononi mwake; hilo karibu liniue.

Kwa hiyo, baada ya kitambo kidogo, baiskeli yake ikasimama upande wa mbele, naye akaingia, akasema, “Halo, Baba,” akakimbia, akanikumbatia.

Nikamshika mikononi mwangu, nami nikasema, “Billy, ulianza hili lini?”

Akasema, “Nini, Baba?”

Nikasema, “Kuvuta sigara.”

Akasema, “Sininii . . .”

Nikasema, “Usiniambie. Unavuta sigara, Billy.”

¹¹ Ndipo akaanza kulia. Nisingeweza kujizuia, nikatoka nikaenda bafuni, nikaketi chini humo, nami nikalia kama mtoto mchanga. Nikawaza, “Mama yake huko Utukufuni, na jambo la mwisho alioniambia, ‘Mtunze Billy.’ Na hapa nimejaribu kuweka mfano mbele zake, halafu kumwona akifanya jambo kama hilo!” Karibu liniue.

¹² Kwa hiyo nikampeleka matembezini, nikasema, “Mwanangu, unatoka huko sasa hivi. Nitakupeleka kwenye shule ya Biblia, hata uwe mpweke jinsi gani.” Na kwa hiyo nikasema, “Nataka unyoshe mikono yako namna *hii*.”

Ndipo akafanya hivyo, akasema, “Kuna nini?”

¹³ Nikasema, “*Huku* ni kushoto na *huku* ni kulia. Sasa, huwezi kuwa unaenda pande zote mbili kwa wakati mmoja. Uko katika umbo la msalaba.” Nami nikasema, “Mradi tu unaenda mkono wa kulia, huenda ukafikiri unaenda vibaya, lakini huna budi kutokea sawa. Huwezi kwenda mashariki na magharibi kwa wakati mmoja; huwezi kuwa unafanya mema na mabaya kwa wakati mmoja.”

¹⁴ Wakati mwingine watu wanaenda vibaya, wakifikiri wanafanya mema, lakini itaishia vibaya. Kwa hiyo sikuzote wazia mema, fanya mema, nawe utafanikiwa, huna budi tu kufanya hivyo. Hiyo ni kweli kabisa. Tenda mema, huo ni wajibu wako kwa Mungu; wazia mema, ujue ya kwamba huna budi kutokea vema; nawe utafanikiwa.

¹⁵ Ndipo sikuzote nilikuwa na msemu mdogo niliowaambia watu niliowaoza. Mnawaona hao mume na mke vijana, nao wanakuja mbele yangu, daima ninawazia juu ya Kristo na Bibi-arusi Wake, ile Karamu kuu ya Arusi ambayo sote tuna shauku ya kuhudhuria.

¹⁶ Na kuwaona kule, wao ni vijana, wachanga, na macho yao maangavu, wakisimama pale kuweka nadhiri hii ya kuwafungamanisha katika safari ya maisha, daima mimi huwaambia kitu kama hiki: “Sasa, mnataka kuwa na furaha, wala hamwezi kuwa na furaha bila Kristo, hakuna nyumba yenye furaha bila Kristo.”

¹⁷ Ninataka tu mnionyeshe moja. Una imani ya kujisingizia, bali huwezi kuwa na furaha bila Kristo. Kweli. La, unaninii tu, unachora moto, kama mtu anayejifanya kuwa Mkristo. Unaweza je kupata joto kwa moto uliochorwa? Moto wa kuchorwa hautapasha joto, inahitaji moto halisi kupasha joto.

¹⁸ Tunaweza kusoma huko nyuma na kuona yale Roho Mtakatifu aliyofanya kwenye Siku ya Pentekoste, hiyo ilikuwa kwenye Pentekoste miaka elfu mbili iliyopita. Kama Moto uo huo hauleti matokeo yale yale siku hizi, Mungu wa kihistoria anatufaa nini kama Yeye si Mungu yeye yule leo?

¹⁹ Ni kama kumlisha vitamini kurumbizi apate kufanya mabawa na manyoya mazuri yenye nguvu, kisha umweke kizimbani. Mabawa yake yanamfaa nini? Unaona? Kama hutahubiri Injili yote, na kuamini kila kitu, na kumpokea Roho Mtakatifu kama ilivyokuwa wakati huo, kuna faida gani kuwa na Biblia kama Yeye si Mungu yeye yule? Mnaona, ni, Yeye hana budi kuwa yeye yule, la sivyo haifai kitu kwenda shuleni na kujifunza theolojia, na kadhalika, kama unataka kumweka huko nyuma kama Mungu wa kihistoria. Ni yeye yule usiku wa leo.

²⁰ Nami daima huwaambia waume na wake wangu wachanga namna hii, kwamba furaha hiyo haijumuishi ni kiasi gani cha mali ya ulimwengu unachomiliki, bali jinsi unavyoridhika na sehemu uliyogawiwa. Hiyo ni kweli, pia.

²¹ Nimeona mume na mke ambao hawakuwa na kitu. Nilioza mume na mke hapa miaka kadhaa iliyopita, sijui jinsi walivyowahi kuniomba niwaoze, lakini huyo mvulana alikuwa ni rafiki yangu. Baba yake alifanya kazi nami katika kampuni ya utumishi wa umma, kijana mwerevu sana, anayeonekana mwenye akili, naye akamwoa binti wa milionea; vifundo vya milango vilikuwa karati kumi na nne za dhahabu nyumbani mwao. Na ilinibidi kufanyizwa mazoezi ya hi—hiyo sherehe kwa muda mrefu sana, nikirudi nyuma pale, na kutupa mchele, na vitu kama hivyo, na kupiga magoti kwenye mto wa hariri. Na loo, sherehe kubwa hivyo!

²² Lakini nilipowaoza, yapata miezi mitatu baadaye, ndugu yangu akaniambia, alikuwa na mume na mke waliokuwa

wanataka kufunga ndoa, ila tu huyo mvulana hakuwa na pesa za kutosha kufunga ndoa. Alikuwa na msichana, lakini hakuwa na pesa za kumlipa mhubiri. Naye akasema, “Vema, ndugu yangu hajawahi kumtoza mtu yeyote chochote.”

²³ Nami, mwajua, nina umri wa miaka hamsini na mmoja, nimekuwa hudumani miaka thelathini na mmoja, na kamwe sijawahi kuchukua matoleo maishani mwangu. Kamwe sijawahi kuchukua... Kamwe sikusudii kufanya hivyo. Kwa hiyo, si—sifanyi hivyo. Ha—haina budi kufanywa, lakini ninaninii tu, chochote mtu yeyote anachonipa ni sawa; wasiponipa, ni sawa, kwa vyovyote vile. Yeye—Yeye anaweza kunyesha chakula kutoka Mbinguni, kwa hiyo ninaliachilia tu namna hiyo. Kwa hiyo, ninamwamini tu. Kamwe sikukosa mlo wowote, nimeahirisha baadhi, lakini sija—sijakosa wowote bado. Lakini daima imekuwa ni vema kumjua Yeye.

²⁴ Kwa hiyo basi wakati hawa mume na mke vijana waliposhuka wakaja, nilimwangalia mvulana huyo aliyesimama pale, katika wakati huo wa kuzorotota kwa uchumi, yeye... maskini suruali kuuu iliyochakaa, na shati kuukuu, ukosi mmoja, kipande cha ukosi kilichofungwa juu kuliko kine, kunyoa nywele, alikuhitaji sana. Maskini msichana huyo mdogo alikuwa ameomba lifti kutoka Indianapolis kuja huku chini, maskini miguu yake ilikanyaga chini, nilijisikia kumnunulia mtoto huyo jozi ya viatu, maskini msichana mdogo mrembo sana.

Ndipo nilipo... Nikasema, “Utampeleka wapi, mwanangu?”

²⁵ Alikuwa na behewa kuukuu huko chini mtoni, ambako kulikuwa na kiwanda cha Dial Ironworks, walikokuwa wakininii, wanakunja chuma kule. Mbona, alikuwa aende kule kuishi kwenye behewa hili.

Ndipo nikasema, “Utafanya nini kama kazi hii ikiisha, kama huna kitu, hata huna chakula?”

Akasema, “Nitampenda vivyo hivyo.” Hiyo ni kweli, ndivyo ilivyo.

²⁶ Vema, siku moja nikashuka nikaenda kuwatembelea marafiki zangu walioishi Silver Hills, na, Herman, nilimjua vizuri sana, Herman Holtz, rafiki msiri wangu sana, alimwoa binti ya E. V. Knight. Nao walikuwa na nyumba nzuri, haikumbidi kufanya kazi tena, alikuwa tu amefaulu, kwa sababu walikuwa na pesa nyingi sana, waliendesha kampuni kubwa za mchanga, na kadhalika, mtoni, na kadhalika.

²⁷ Nami nikaenda kule kumwona kwa wakati ufaao, nadhani, mmoja alikuwa ameketi kwenye kona moja, na mwingine kwenye nyingine, wakibishana. Nao walikuwa wameenda kwenye dansi usiku uliotangulia, karamu fulani, na kulikuwako na mwanamume fulani aliyecheza dansi pamoja naye, na

kumkasirisha mke, ama, kumkasirisha mume. Na basi hiyo hapo, walikuwa wakizozana.

²⁸ Basi nilipofika barazani, mnajua walifanya nini? Wakakimbia, wakashikana mikono, na kuja mlangoni, kasema, “Halo, Ndugu Branham.” Sasa, huo ni moto uliochorwa, ambao haudumu, huo haufai kitu.

Nikasema, “Vema, nina furaha kuwaona ninyi nyote.” Nikasema, “Mna furaha?”

“Loo, naam, mpenzi, sivyo?”

²⁹ Nikajua papo hapo. Nilikuwa tayari nimewasikia nilipoikaribia hiyo nyumba. Mnaona? Nilijua walikuwa wakizozana. Vema, wakaendelea, nawe ungeweza kuona haikuwa sawa, hiyo roho haikuonekana nzuri.

³⁰ Siku moja nikawazia ningetafuta kujua kilichowapata mume na mke niliowaoza, na waliishi katika behewa. Kwa hiyo, nilikuwa nikifanya kazi katika Kampuni ya Utumishi wa Umma, nilikuwa fundi wa nyaya kule kwa muda wa miaka kumi na saba, nikashuka chini mtoni, na kidogo nikajifanya kama mnaafiki, nikavaa njumu zangu na usalama, nikashuka nikifuatilia huo mto kana kwamba nilikuwa nikikagua nguzo.

³¹ Nikapanda juu kisiri, ndipo nikaona Chevrolet yake kuukuu huko nje huku taa za mbele zimefungwa kwa nyaya za kufungia, nami nikaelekea mlangoni, nikawasikia wakizungumza. Naye alikuwa amecha kazi kutoka PWA, chochote ilichokuwa, walifanya kazi kule, naye alikuwa akifanya kazi katika kampuni fulani ya mbao huko juu, akipata kama dola nane ama kumi kwa juma, hizo zilikuwa ni pesa nzuri sana.

³² Na kwa hiyo, alikuwa . . . walikuwa wamechukua lile behewa kukuu wakalibandika magazeti juu na misumari yenye vichwa vipana. Ni nani anayejua misumari yenye vichwa vipana ni nini? Kwani unatoka sehemu gani ya Kentucky, mwanangu? Wakachukua kadibodi, wakaibana kwa msumari, na kuipigilia tu ukutani, unaona, pamoja na karatasi na magazeti. Alikuwa amelea makatoni yaliyochakaa, nao walikuwa wametengeneza meza kutokana nayo.

³³ Lakini, ndugu, kama niliwahi kuona Mbingu duniani, ilikuwa ndiyo hiyo. Mke alikuwa ameketi pajani mwake mume, alikuwa ametoa kofia yake kuukuu, akabonyeza sehemu yake ya juu, alikuwa amemwaga ndani mshahara wake, nao walikuwa na *kadhaa* zimewekwa hapa za chakula, na *kadhaa* za bima, na *kadhaa* za *hapa*. Naye akasema, “Mpenzi, ninataka sana kukununulia nguo hiyo.” Ninaamini ilikuwa yapata dola moja na robo, kitu kama hicho.

Akasema, “Lakini, Mpenzi, sisi . . . Ninathamini hilo.” Mkono mmoja umemkumbatia namna *hiyo*.

34 Naye akamtazama. Nami nilikuwa nimesimama pale kama mnafiki nikimwagalia, mwajua. Na, kwa hiyo, wakaanza kuhesabu pesa hizi, nao hawakuwa na za kutosha kulipia yote. Naye akasema, “Vema, nilifanya hizo... Nimekuwa nikijaribu sana. Maskini gauni hilo limetundikwa dirishani huko juu, ni dola moja na robo. Hivi tusingeweza tu kuachilia bima, ama chochote kile?”

Akasema, “La, Mpenzi, nathamini hilo.” Loo, akamkumbatia.

35 Nami nikasimama pale na kugeuka *hivi* na kutazama juu ya kilima, nami ningeweza kuona nyumba ya huyo mwingine, minara mirefu juu ya hiyo nyumba. Nikawaza, “Tajiri ni yupi? Ungetaka kuchukua yupi, Billy, kama ulikuwa unaenda kuchagua?” Hebu niwe na mke halisi, wa kweli, anayenipenda, hebu niishi hapa chini kwenye behewa, kwa kuwa nawaambia, furaha na utoshelevu, pesa haziwezi kununua, pesa haziwezi kununua upendo, hivyo ndivyo vitu halisi.

36 Vema, mimi huyu hapa ninaendelea kuzungumza, jambo la kwanza wakati utakuwa umeenda. Na hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu, na kuzungumza na Bwana sasa.

37 Baba yetu wa Mbinguni wa Thamani, tunakaribia vivuli vya rehema Yako katika Jina la Bwana Yesu, tukijua jambo hili, ya kwamba Yeye ametuahidi ya kwamba tungeweza kufanya mahojiano na Wewe wakati wowote, na tuwe na hakika ya kwamba tungepokea kama tungekuja katika Jina Lake. Kwa hiyo, Bwana, hatuna haki, hatuna jina, hakuna chochote tulicho nacho katika maisha haya, ama tujuacho, hapa duniani ambacho tungeweza kukikaribia Kiti Chako cha Enzi, ila tu kwa Jina la Yesu.

38 Nasi tunakuja kwa unyenyekevu, Bwana, tukikupa Wewe sifa ya mioyo yetu kwa kumtuma Yeye duniani, tupate kuwa na njia hii kuu ya kuingia katika Uwepo Wako kwa Damu iliyomwagika pale Kalvari, na tungekuwa na hakikisho kwamba Wewe utayasikia maombi yetu.

39 Tunakushukuru, Baba Mtakatifu sana, kwa yote ambayo umekuwa kwetu katika mkutano huu kufikia umbali huu. Tumeuona mkono Wako mkuu, wenye nguvu ukishuka kwenye kusanyiko na kuwashawishi wenye dhambi kwamba walikuwa wamekosa, kuwaona wakija madhabahuni katika toba na—na kukukubali Wewe kama Mwokozi na Bwana wao wa pekee. Tumewaona hao, Bwana, waliokuwa wagonjwa na wanaoteseka, wakiondoka humu jengoni wazima, wakisimama kutoka kwenye viti vya magurudumu na kuondoka. Tunakushukuru, Baba wa Mbinguni, kwa ajili ya mambo haya.

40 Ndipo tumeona Roho Wako Mtakatifu akilitia upako kusanyiko hili, mpaka kusingekuwa na siri moja moyoni

pasipo Yeye kuifanya ijulikane, akitimiza Maneno yale yale aliyoahidi kwamba yangetukia. Ee, Baba yetu, uturehemu sisi viumbe tusiostahili. Hatuwezi kukuelezea Wewe, Bwana, jinsi tunavyotaka, jinsi tunavyokupenda na kukuthamini Wewe kwa ajili ya mambo haya.

⁴¹ Tukijua ya kwamba katika saa hii yenye giza ya matukio ya mwisho ya historia ya ulimwengu, wakati watu wamechanganyikiwa, na watu wanakimbia kutoka kanisa hadi kanisa na kutoka mahali hadi mahali, wakibadilishana barua na kuzibeba mahali mahali, na hata hivyo sisi tulipata mahali hapo pa kudumu, mahali pa kupumzikia katika Mungu.

⁴² Jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya Roho Mtakatifu anayetupa faraja katika saa hii! Nasi tunaomba, Baba, ya kwamba atakaa pamoja nasi milele, wakati vivuli vikizidi kurefuka, nasi tunajua jua linatua kwenye ustaarabu.

⁴³ Mungu, tungeomba sasa kwa ajili ya taifa hili letu kuu ambalo liko katika wakati wa kubadilishwa kwa marais. Huenda likaonekana kama jambo jepesi, lakini, Mungu, huenda likabadilisha kikomo cha taifa hili. Ee Bwana, Wewe uliyeweza kuwachagua manabii na—na kuwatia mafuta wafalme, tunaomba ya kwamba Roho Wako Mtakatifu atamtia mafuta mtu anayefaa kwa ajili yetu katika saa hii. Tujalie, Bwana. Mahali ambapo mikusanyiko mikubwa inaendelea kwa pande zote mbili, Baba, tunatambua ya kwamba Wewe huvutiwi na vyama, ni watu unaoweza kuwa na imani nao. Kwa hiyo ninaomba, Baba, ya kwamba mahali fulani hapo kwamba watamchagua mtu anayefaa kwa saa hii.

⁴⁴ Tunajua ya kwamba wakati hauna budi kuja ambapo mtu asiyefaa atachaguliwa, pia. Kwa hiyo tunaomba, Baba, ya kwamba utatupa muda zaidi kuwaleta waliopotea. Jalia, kama kuna yeyote wa hao hapa usiku wa leo, tunapoona vivuli vikizidi kurefuka, jalia waje kwa utamu kwa Bwana Yesu na waokolewe. Waponye wagonjwa na wanaoteseka, liimarishe Kanisa. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina Lake. Amina.

⁴⁵ Ndugu Borders, aliyesoma Maandiko dakika chache tu zilizopita, wakati mwingine ninayasoma mwenyewe, na nilifikiri usiku wa leo kwamba ningemwomba Ndugu Borders anisomee, Ufunuo mlango wa 3, kifungu cha 14 na kuendelea kwa mlango huo.

⁴⁶ Kwa kuwa baada ya wao kuyasoma Maandiko ndipo wimbo unaanza kuimbwa wakati nilipoishika mikono ya Ndugu Mercier aliyesimama pale nyuma, alisema, “Kwa nini ukafanya hivyo?”

Nikasema, “Usikilize wimbo huo.”

Akasema, “Ninaona unachomaanisha. ‘Amini tu,’ amini tu yale yanayoandikwa.”

47 Ujumbe huu ni ujumbe kwa Wakati huu wa Kanisa, Wakati wa Kanisa la Laodikia, ambao ulikuwa ni wakati wa uvuguvugu wa kanisa. Nami ninamtumainia Mungu, usiku wa leo, kutoa kutoka kwenye fungu nitakalochagua ambalo ni kifungu cha 20. Kutoka kwenye fungu hili, ninataka kusema hivi, ambalo linasema:

Tazama, nasimama mlangoni, nabisha: mtu akiisikia sauti yangu, na kunifungulia Mimi, nitaingia kwake, na . . . nitakula pamoja na yeye, na yeye pamoja nami.

48 Ninataka kuchukua somo pale la *Mlango Ndani Ya Mlango*.

49 Sasa, hili hakika ni tukio lisilo la kawaida, na ni somo lisilo la kawaida, lakini mnajua, Mungu si wa kawaida. Mungu hufanya mambo kwa njia isiyo ya kawaida, katika wakati usio wa kawaida, katika mahali pasipo pa kawaida, wakati mwingine kwa watu wasio wa kawaida. Mungu si wa kawaida, Yeye hufanya yasiyotarajiwa mara nyingi.

50 Halafu huenda tukasema, tena, kwa kusanyiko hapa la watu mia kadhaa, “Hilo si ni somo dogo la kufanya, *Mlango Ndani Ya Mlango*, kuchagua yapata maneno saba kutoka kwenye moja ya vifungu hivyo?”

51 Vema, si wingi wa kitu chochote unaojalisha, ni ubora unaojalisha.

52 Wakati fulani uliopita kulikuwako na ha—hadithi ndogo niliyosikia, ya mvulana mdogo aliyekuwa akipekua-pekua darini, naye, kwenye kasha kuukuu, akapata stempu ya posta, jamaa mdogo, manjano kwa uzee. Naye maskini jamaa huyo alikuwa akiwazia aiskrimu niani mwake, kwa hiyo alikuwa na mkusanya stempu mtaani ambaye alimkimbilia kumwuzia stempu hiyo ya posta, alidhani angepata senti tano, bei ya koni ya aiskrimu.

53 Wakati yule mkusanyaji alipoiweka chini ya darubini, akaiangalia, alisema, “Nitakupa noti ya dola.” Mbona, harakati za biashara zilifungwa upesi sana, kwa sababu alifurahia kupata hii dola. Huyu akashuka kwenda mtaani akiotea koni kadhaa za aiskrimu, niani mwake.

54 Baadaye, ninasikia ya kwamba mkusanyaji huyu aliuzia stempu hii kwa dola mia tano. Ndipo ikatoka hapo ikafikia mamia na mamia ya dola. Nami ninasahau sasa hiyo stempu ina thamani gani. Karatasi iliyoandikiwa hata halikufaa kuokotwa, haikuwa hiyo karatasi, cha muhimu ni kile kilichokuwa kwenye hiyo karatasi.

55 Wala si ukubwa wa somo langu usiku wa leo, si thamani ya karatasi iliyoandikiwa, ni kile kilichoandikwa kwenye hiyo karatasi: Ni Neno la Mungu aliye hai, toleo la msamaha. Msamaha, ni kusamehe, Neno linasamehe kila mwanamume, ama mwanamke, ama mvulana, ama msichana atakayelipokea.

⁵⁶ Miaka kadhaa iliyopita katika vita vya wenyewe kwa wenyewe, ama yale mapinduzi, ilikuwa mojawapo, ninaamini ilikuwa ni wakati wa Abraham Lincoln, naam, ambapo palikuwa na askari aliyekuwa amefanya vurugu, naye alikuwa ametoroka wakati wa vita, akakwepa wajibu wake. Nao wakamkamata huyo mtu, nao wakamshtaki mahakamani na kumpata na hatia. Nayo hukumu ilikuwa ni kupigwa risasi na kikosi cha wapiga risasi.

⁵⁷ Basi palikuwa na mtu aliyewaza sana juu ya jamaa huyu kijana. Alikuwa mvulana mwenye wasiwasi, mwenye fadhaa, basi wakati maskini magobori na mizinga ilipoanza kufyatuka, alitoroka tu, kwa sababu aliogopa mno. Lakini alikuwa amekwepa wajibu wake, naye alikuwa anaenda kuuawa, mauaji yake yakapangiwa siku fulani.

⁵⁸ Ndipo rafiki yake akamwendea rais wa Marekani, mwenye neema Abraham Lincoln. Ndipo maskini mzee Abe, alipokuwa akiingia kwenye chumba cha hoteli, rafiki huyu alimkimbilia, naye akasema, “Bw. Lincoln,” naye akasema, “najua wewe ni Mkristo, wewe ndiwe amiri Jeshi mkuu. Basi mtu fulani huyu ana hatia ya kile walichomshitakia, lakini hali zake, aliogopa, yeye ni mtu mzuri. Nami najua huamini katika kuyachukua maisha ya mtu. Neno lako likiwekwa kwenye kipande cha karatasi, maisha yake yataokolewa. Hata kama inambidi kukaa katika gereza la shirikisho, usiache auawe, alikuwa mvulana mzuri, nilimjua, nililelewa katika ujirani pamoja naye.”

⁵⁹ Maskini mzee Abe alijitwalia kipande cha karatasi na kuandika maneno machache tu pale, “Msameheni mtu huyu, Abraham Lincoln.”

⁶⁰ Loo, mvulana huyo akarudi mbio kwenye seli za gerezani, naye akamwonyesha rafiki yake, akasema, “Umesamehewa kabisa!”

Akasema, “Usinidhihaki, huku ukijua nitakufa asubuhi.”

Akasema, “Huyu hapa rais wa Marekani, amiri jeshi mkuu, alitia sahihi msamaha wako.”

⁶¹ Ndipo mvulana huyo akakiangalia, kasema, “Hicho ni kipande tu cha karatasi, hakifai kitu. Unajaribu kukifanya kifo changu kibaya zaidi kuliko kilivyokusudiwa kuwa. Sitaupokea.”

⁶² Naye akarudi ndani kwenye seli, na akakataa kukiangalia hicho kijikaratasi tena, kwa sababu alisema, “Kama Bw. Lincoln angelitia sahihi msamaha wangu, ungekuwa na—na ninii zote—anwani, na kadhalika, na muhuri wake juu yake, na kadhalika, kwa hiyo basi sitaupokea kwa sababu ni dhihaka tu.”

⁶³ Kesho yake asubuhi huyo mtu akafa mbele ya kikosi cha wapiga risasi. Sasa, itakuwaje? Kuna yule amiri jeshi mkuu wa Jeshi anayesema ya kwamba mtu huyu amesamehewa, na sasa amepigwa risasi na kikosi cha wapiga risasi. Sasa tutafanya

nini? Ilisikizwa katika mahakama ya shirikisho ya taifa letu, na huu hapa ndio uliokuwa uamuzi wa Mahakama Kuu, ama mahakama ya shirikisho, ilisema, “Msamaha si msamaha, isipokuwa upokewe kama msamaha.”

⁶⁴ Kwa hiyo Neno hili usiku wa leo ni msamaha kwa kila mtu atakayelipokea, bali kama hutaki kulipokea, si msamaha. “Tazama, nasimama mlangoni, nabisha, mtu yeyote akiisikia Sauti Yangu, na kunifungulia, nitaingia kwake.” Ni mwaliko wa jinsi gani!

⁶⁵ Kuna mchoro maarufu, ninamsahau yule msanii wa Kiyunani aliyeuchora, wengi wenu huenda mkajua jina la msanii huyo, lakini alitumia maisha yake yote akichora picha ya Kristo mlangoni, akibisha.

⁶⁶ Na wakati, picha zote kuu kabla hazijakuwa picha maarufu, ilibidi zikaguliwe na wakosoaji, na wakati wakosoaji walipokuwa wakikosoa, ama kujaribu kupata kitu cha kuikosoa picha hiyo, mkosoaji mmoja akamwambia, “Bwana, mchoro wako ni mchoro mzuri sana. Unaonyesha ya kwamba Kristo anayo taa mkononi Mwake, anapomjia mwenye dhambi gizani. Anakuja usiku, hakuna kitu ningaliweza kusema kuhusu hilo, kwa kuwa hapo ndipo Yeye anapomjia mwanadamu, ni wakati anapokuwa gizani. Na mwonekano wa uso Wake anapobisha mlangoni kwa matarajio ya kusikia mtu fulani ndani akiitikia Sauti Yake, ama, kubisha Kwake.”

⁶⁷ Kisha kasema, “Yote imechorwa vizuri na kuonyeshwa hapa, lakini,” kasema, “kuna kitu kimoja ambacho lazima niseme ambacho ulisahau.” Akasema, “Angewezaje kuingia? Huna komeo mlangoni.”

Ndipo huyo mchoraji akasema, “Huo ndio ukosoaji wako?”

Akasema, “Naam.”

Akasema, “Bwana, niliichora picha hii hivi.” Akasema, “Unaona, hii ni aina tofauti ya mlango, komeo liko ndani.”

⁶⁸ Hivyo ndivyo ilivyo, Kristo hawezi, kwa mapenzi Yake Mwenyewe, kuufungua mlango na kuingia, anaweza tu kubisha, halafu wewe ufungue mlango, komeo ni juu yako. Anaweza kubisha, lakini inakubidi wewe kufungua. Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo.

⁶⁹ Na ndipo tunapowazia juu ya mtu anayebisha mlangoni, si jambo lisilo la kawaida. Jambo, sehemu muhimu inayojalisha, si huyo mtu anayebisha mlangoni, ni umuhimu wa huyo mtu mlangoni. Watu wengi hubisha mlangoni kila siku, bali ni umuhimu wa huyo mtu.

⁷⁰ Naye mtu abishaye ni, anafanya nini, kwa vyovyote vile? Anajaribu kuninii... yeye ni... Labda ana ujumbe wako, ama labda anataka umfanyie jambo fulani, ama labda una kitu anachotaka. Kuna sababu fulani ya yeye kujaribu kuingia

mlangoni, akijaribu kuvutia usikivu wako, akijaribu kukufanya ufungue aweze kuhojiana nawe, akijaribu kuzungumza nawe kwa muda kidogo tu. Na kumekuwako na kubisha mara nyingi kwenye mlango mingi na watu wengi mashuhuri.

⁷¹ Kwa mfano, katika siku za Rumi, wakati Rumi ilipoutawala ulimwengu uliojulikana, vipi kama yule mfalme mashuhuri wa Rumi, Kaisari, angeshuka kwenye nyumba ya mkulima mdogo, ambapo ma—maskini aliishi, naye angebisha mlangoni? Naye huyo maskini angeangalia pembeni na kuona ya kwamba alikuwa ni mfalme mkuu wa Rumi akibisha mlangoni pake. Unafikiri maskini mkulima huyo mdogo angewazia nini? Ingekuwa ni heshima jinsi gani kwa mfalme huyu wa Kirumi kuja mlangoni pa maskini mmoja na kubisha mlangoni pake!

⁷² Huyo mkulima mdogo angeenda mlangoni, afungue mlango, na kusema, “Mfalme mkuu wa Rumi, unaiheshimu nyumba yangu! Umenipa heshima kubwa, bwana mwema. Karibu kwenye nyumba yangu ndogo. Na kama kuna kitu chochote hapa nilicho nacho ambacho unataka, umekaribishwa hata na zaidi kwa chochote nilicho nacho. Kama kuna kitu chochote ambacho bwana wangu anataka kwangu, kwa furaha nitamtolea hata maisha yangu.” Loo, ingekuwa ni heshima kwa nyumba hiyo kwa m—mfalme wa Rumi kuitembelea hiyo nyumba.

⁷³ Au katika vile vita vya mwisho, huyu marehemu Adolf Hitler, mtawala mkuu wa Ujerumani, katika siku za ufanisi wake mkuu na udikteta wake juu ya Ujerumani, vipi kama huyu Adolf Hitler mashuhuri alishuka kwenda kwenye nyumba ya askari, askari wa miguu wa jeshi lake na kubisha mlangoni? Ndipo maskini askari huyu akainua pazia na kuona ya kwamba ilikuwa ni yule mtawala mkuu wa Ujerumani amesimama mlangoni, ni heshima iliyoje! Jinsi angeweza kujigamba na kuwaambia askari wengine, “Hitler alikuja mlangoni pangu. Nilikuwa mgeni mheshimiwa. Niliheshimika kutembelewa na Hitler nyumbani kwangu.” Angefurahia kusema hivyo.

⁷⁴ Angefungua mlango, asimame miguu sawa, na kupiga saluti ya Kijerumani, na kusema, “Bwana, hivi kuna chochote ambacho kiongozi mkuu wa Ujerumani anataka kutoka kwa mtumishi wake? Niko tayari hata kufa kwa ajili yako. Kuna kitu chochote nyumbani mwangu unachotaka? Unaweza kuchukua chochote nilicho nacho. Ni heshima iliyoje kwangu! Leo hii ni siku yangu ya kutawazwa kujua ya kwamba mtawala mkuu wa Ujerumani amesimama mlangoni pangu, nami ni askari tu wa miguu, askari tu jeshini. Nawe umeniheshimu, bwana, hata kusimama kwenye uwanja wangu.” Mbona, bila shaka, ingekuwa ni heshima.

⁷⁵ Au vipi, hata usiku wa leo, kama Rais wetu mheshimiwa na mpendwa sana Dwight Eisenhower, kama angekuja kwenye... nyumba yako, kama angekuja kwenye—kwenye nyumba ya

mwanademokrasia aliye bora zaidi katika bonde hili, ingawa ungetofautiana naye katika siasa, ingekuwa ni heshima kwako, kwa kuwa yeye ni mtu muhimu, angali ndiye rais wa Marekani, naye ni mtu anayeheshimika sana. Huenda usikubaliane naye katika siasa, lakini hata hivyo yeye ni mmoja wa Wamarekani mashuhuri sana leo hii, ni Rais wetu Dwight Eisenhower.

⁷⁶ Vema, kama angekuja nyumbani kwako asubuhi na kubisha mlangoni, ungekuwa mtu aliyeheshimika. Kila gazeti huko Oregon lingeandika makala hayo, kwamba Rais Dwight Eisenhower alikuja nyumbani kwako. Jinsi kila mtu angewazia jinsi alivyokuwa mnyenyekevu kuja nyumbani kwetu, sisi watu maskini, yeye rais wa Marekani. Ingekuwa ni heshima kubwa kwako kumpokea. Ungesema, “Bw. Eisenhower, ingia nyumbani kwangu. Unabariki...Uwepo wako unatubariki. Umetuheshimu.”

⁷⁷ Na kesho, magazeti yangesema, na re—radio, na televisheni zingeandika makala hiyo: *Rais Eisenhower Aja Kwenye Maporomoko Ya Klamath, Na Kumtembelea M—Mtu Maskini*. Mbona, angejinyenyekeza sana kufanya hivyo. Na lingekuwa jambo kuu kwako kumpokea, nawe ungefurahia kumpa shauku zake ambalo lingekuwa ni jambo kuu.

⁷⁸ Ama hivi majuzi tu, wakati malkia wa Uingereza, alipokuja hapa kutembea, kama angekuja kwa baadhi yenu wanawake hapa, aje nyumbani kwenu, na kusema, abishe mlangoni, nawe ungeenda mlangoni, naye angesema, “Mimi ni malkia wa Uingereza.”

⁷⁹ Ingawa yeye ananinii...huna uhusiano wowote naye, milki yake haiko Marekani, lakini hata hivyo, yeye ndiye malkia mkuu sana wa duniani tuliye naye, yeye ni mwanamke muhimu, ingekuwa ni heshima kwako kumkaribisha malkia wa Uingereza, ungesema, “Karibu, Malkia. Nawe unaiheshimu nyumba yangu.”

⁸⁰ Kama angeomba kitu chochote, vipambo vidogo, au kifaa ulichokuwa nacho ukutani, ungefikiri ilikuwa ni heshima kumpa huyo malkia wa Uingereza. Yeye ni mwanamke mashuhuri.

⁸¹ Siku moja huko Kanada, ndugu na rafiki yangu mpendwa, Daktari Ern Baxter...Wakati marehemu Mfalme George na malkia waliposhuka kuja barabarani, tuliambiwa kwamba alikuwa akiugua vibaya sana vidonda vya tumbo na mnyanyuko wa viungo mgongoni mwake; hiyo ilikuwa kabla hatujamwomba huko London. Basi alikuwa anateseka sana siku hiyo, bali aliketi pale kwenye kiti hicho cha behewa, kishujaa tu, huku malkia wake mpendwa ameketi karibu naye, amevaa vazi lake la jioni la bluu, walipokuwa wakipita. Naye Bw. Baxter akasema alipowaangalia, alisema alitetemeka tu na kulia.

Nami nikasema, “Kwa nini, Ernie?”

Akasema, “Mfalme wetu na malkia wetu walikuwa wakipita.” Kasema, “Hiyo, hakika, ilinifanya nilie kwa furaha.”

⁸² Nikawazia, “Kama kupita kwa mfalme wa Uingereza kungemfanya Mkanada alie kwa furaha, itakuwaje wakati Mfalme wa Utukufu atakapokuja?” Itakuwa na matokeo ya jinsi gani kwa Kanisa la Mungu aliye hai tutakapomwona Yesu!

⁸³ Hakika, kama angebisha mlangoni pako, ungefikiri ilikuwa ni heshima kumkaribisha malkia, na lingekuwa ni jambo kuu kwako kufanya hivyo. Lakini, loo, ungetoa heshima ngapi kwa jambo hilo? Lingekuwa ni jambo la heshima jinsi gani! Lakini sikilizeni, kuna Mtu anayekuja milangoni, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, anabisha mlangoni mingi zaidi kuliko wafalme wote na watawala waliowahi kuwako ulimwenguni. Ni nani aliye mkuu na muhimu kuliko Yeye? Na ni nani anayekataliwa zaidi kuliko Yeye anavyokataliwa?

⁸⁴ Unafikiri kama Kaisari angekataliwa, angefanya nini? Mbona angalimfanya mtu huyo auawe, na ninii yake—na nyumba yake iteketezwe, na mke wake na watoto wake kuteketezwa. Hitler angemmwigia askari huyo petroli na kuteketeza maiti yake. Lakini Yesu anaendelea kurudi na kubisha mlangoni, anakataliwa usiku mmoja, anarudi usiku mwingine, ukimkataa tena, Yeye atarudi tena.

⁸⁵ Na kama malkia angekuja kukutembelea, ama rais wetu, ama mtu fulani mashuhuri, hapana shaka wangekuwa wanataka fadhili kutoka kwako, bali Yesu hataki fadhili kutoka kwako, anajaribu kukuletea Uzima wa Milele. Yeye anajaribu kuziokoa nafsi zenu na kuzimu ya ibilisi, na maangamizi ya Milele, na kutengwa na Uwepo wa Mungu, na hata hivyo tunamkataa.

⁸⁶ Na kama ingekuwa ni unyenyekevu kwa rais wa Marekani kuja nyumbani kwako, hata hivyo Mfalme wa Utukufu, Bwana Yesu, anamshukia mtu maskini kuliko wote nchini, kwa mwuza pombe haramu, kwa walevi barabarani, kwa mwanamke mzinzi, kwa mtoto asiyetii, kwa yeyote ambaye Yeye anaweza kumjia na kubisha mlangoni pake, Yesu anakuja na kubisha. [Ndugu Branham aligongagonga mimbarani—Mh.]

⁸⁷ Haidhuru wewe ni duni jinsi gani, jinsi ulivyo mdogo, jinsi ulivyo mtovu wa uadilifu, jinsi usivyo na adabu, umefukuzwa mbali kiasi gani kutoka kwa jamii, hata hivyo Mwana wa Mungu aliye hai anakupenda na anabisha mlangoni pako, siku baada ya siku na usiku, nawe unamkataa. Hiyo ni mbaya sana.

⁸⁸ Hata haionekani ni akili timamu kufanya jambo kama hilo, kumkataa Mwana wa Mungu Ambaye anakuja, si kuchukua kitu kutoka kwako, bali kukuokoa na maangamizi, halafu anakataliwa. Ni tamasha la kusikitisha jinsi gani! Haionekani sawa kiakili kumkataa, si sawa kiakili kumkataa. Kumkataa Mwana wa Mungu anapobisha mlangoni pa moyo wako ni kurukwa na akili, na hata hivyo, Yeye hukataliwa, na atarudi.

Sasa, huenda ikawa kwamba ungeniambia, “Hebu kidogo, Mhubiri, niliufungua moyo wangu muda mrefu uliopita na kumruhusu Bwana Yesu aingie.”

⁸⁹ Vema, hakika nina furaha ulifanya hivyo, na labda hivyo ndivyo ulivyofanya, ukafungua moyo wako na kumruhusu aingie. Lakini *hayo tu* ndiyo uliyofanya? Mungu anataka kufanya jambo lingine. Angalia hapa katika Maandiko, “Nasimama mlangoni, nabisha, mtu akifungua, nitaingia na kula pamoja naye.”

Loo, unasema, “Nilimkubali kama Mwokozi wangu.”

⁹⁰ Vema, labda ulifanya hivyo, lakini hilo halitoshi, Yeye anataka kuwa Bwana wako. Ulifurahi kumruhusu awe Mwokozi wako, hakuna mtu anayetaka kwenda kwenye maangamizi ya Milele, hakuna mtu anayetaka kwenda ku—ku...kuzimuni. Lakini unataka kuepuka kuzimu, bali hutamruhusu awe Bwana wako. Anataka kuingia apate kuwa Bwana, na *Bwana* ni mtawala, umilikaji. Anataka kukumiliki, maana wewe si mali yako mwenyewe, ulinunuliwa kwa gharama. Anataka kukutawala.

⁹¹ Loo, umesema kwa furaha, “Karibu, Bwana, usiniache niende kuzimuni.”

⁹² Lakini vipi kama nikija nyumbani kwako, na kubisha mlangoni nami na—naamini hamnijui, ninyi, wengi wenu hamnijui, lakini kwa kuwa tu ni mhudumu, labda ungenikaribisha ndani, naamini ungenikaribisha. Ungesema, “Karibu, Ndugu Branham.”

⁹³ Vema, kama ukinikaribisha ndani, ningejisikia kana kwamba hiyo ilikuwa tu kama nyumbani kwangu. Kama nikija nyumbani kwako, nawe unikaribishe tu ndani, useme, “Sasa, ngoja kidogo, ingia, lakini simama hapa kwenye mlango huu, usiende mbele zaidi.” Mimi—mimi...Afadhali hata usinikaribishe ndani, maana nisingejisikia vizuri.

⁹⁴ Ukija nyumbani kwangu, na useme, “Ndugu Branham, nilikuwa kwenye mkutano wako wa Oregon huko kwenye Maporomoko ya Klamath, nami ni—nimesikia umerudi hivi punde, kwa hiyo nilifikiri ningekuja.”

Ningesema, “Ingia.”

Useme, “Asante.”

Nami ningesema, “Usiende mbali zaidi ya *hapo* hata hivyo, wewe kaa *papo hapo*.”

⁹⁵ Kama nikiwahi kuwakaribisha nyumbani kwangu, umekaribishwa popote nyumbani kwangu.

⁹⁶ Unajua, baada ya kuingia ndani ya mlango wa moyo, mwajua, kuna milango mingine midogo mle ndani, milango mingi midogo ndani ya nyumba. Nenda uchukue chumba kidogo

hapa, na chumba kidogo *hapa*, na chumba kidogo *hapa*, kuna milango kadhaa. Watu wengi wako tayari kumkaribisha Bwana moyoni mwao, maana hawataki kwenda kuzimuni, bali wao . . . hawataki Yeye awe Bwana anapoingia.

⁹⁷ Vema, kama nikiingia nyumbani mwako, useme, “Karibu ndani, Ndugu Branham,” vema unajua kile ningefanya? Ningeingia, niende kwenye friji, na kujitwalia kipande cha jibini, na soseji, na kujikatia kipande cha kitunguu, na kujikatia mkate, na kuupaka haradali, na saladi, na kadhalika, niende nivue viatu vyangu, na kujilaza kwenye kochi ama kitandani, na kula sandwichi hii, na—na kunywa kinywaji baridi kama ulikuwa nacho, na, loo jamani, ningejifanya tu nyumbani, nitundike kofia yangu. Kama ulisema, “Karibu,” ningeamini neno lako.

⁹⁸ Lakini kweli tunamkaribisha Bwana Yesu, tukaliamini Neno Lake? Basi, hivi anaweza kuamini neno letu? Sasa, hebu na tuangalie kwenye baadhi ya milango hii midogo moyoni kwa dakika chache zijazo.

⁹⁹ Mlango mdogo wa kwanza unapougeukia upande wa kulia, tunganese, na unapoingia moyoni, kuna mlango pale unaoitwa, “Kiburi.” Loo, jamani! Unajua, hutaki kumjua Yesu akisimama kwenye mlango huo, maana Yeye anakuondolea hiyo yote, anaufungua mlango huo mara moja. Loo, kama ungeweza . . .

¹⁰⁰ Unasema, “Sasa, ngoja kidogo, Yesu, Wewe unaweza kuniokoa, bali usianze kuvuruga majivuno yangu. Sasa, kama itanibidi kusimama pale na kutenda kama baadhi ya hao watu wafanyavyo, nisingeweza kufanya hivyo,” basi Yeye hajakaribishwa.

¹⁰¹ Hebu niseme hivi: Wala Yeye hatakaa muda mrefu sana, tegemea tu hilo. Nisingekaa kama ungeniambia hivyo, usingekaa kama ningekwambia hivyo, kwa hiyo Yeye hatakaa kama tukimwambia hivyo. Kiburi!

¹⁰² “Vema sasa, nakwambia, Ndugu Branham, kama itanibidi kushuka hapo kwenye hiyo madhabahu, kulia, kumfanya rafiki yangu wa kike anichukie, mpenzi wangu wa kiume anikatae, mke wangu aniambie mimi ni mtakatifu anayejibingirisha, mume wangu aseme nimerukwa na akili, sasa, kama Wewe utafanya jambo hilo, Yesu kaa nje!” Hivyo ndivyo wanavyosema hasa, sana. “Sitafanya hivyo.”

¹⁰³ Hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikizungumza na, hapa Oregon, na maskini msichana mmoja aliyekuja kunihoji, naye alikuwa na ki—kitabu kidogo mkononi mwake, naye alikuwa anaenda kuhoji kwa niaba ya gazeti. Nami nikasema, “Umeihudhuria hiyo mikutano?”

Akasema, “Nilikuwa huko jana jioni.”

Nikasema, “Ulionaje kuhusu huo mkutano?”

Akasema, “Sijawahi kusikia wapumbavu wengi hivyo maishani mwangu mwote.”

¹⁰⁴ Nikasema, “Je, . . . ? Ninajua sasa kwamba wewe si Mkristo.” Naye akaniambia alikuwa mfuasi wa kanisa la aina gani. Ndipo nikasema, “Ningetaka kukuonyesha, dada yangu, ya kwamba katika Biblia kwamba mungu wako wa kike, Mariamu, unayemwomba, ilimbidi mwanamke huyo kuja Pentekoste na kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kuyumbayumba chini ya nguvu zake kama mlevi, kabla Mungu hajamruhusu kuja Mbinguni. Na kama Mungu alimfanya bikira Mariamu aliyebarikwa afanye hivyo, utawezaje kufika mle kwa chochote pungufu?”

¹⁰⁵ Alimzaa, akamzaa Bwana Yesu kibikira, lakini hata hivyo, asingeweza kuingia, mpaka alipokuwa amejazwa na Roho Mtakatifu. Nikaweka kidole changu kwenye Maandiko, wala huyo mwanamke hata hakuwa na ujasiri wa kuyaangalia. Nena kuhusu ushenzi!

Hapo, alipogeuka na kuniangalia, alisema, “Siamini hilo.”

¹⁰⁶ Nikasema, “Je, unaamini Biblia? Biblia ilisema ya kwamba Mariamu, Yohana Mtakatifu, Mtakatifu. . . hao watakatifu wengine wote, Petro na hao wote, ilibidi waende kule juu na kubaki mpaka Roho Mtakatifu aliposhuka, na wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, na kuanza kugugumiza kwa midomo yao, kisha wakaanza kunena kwa lugha zingine, na kutenda kwa njia ambayo hata wasikilizaji waliokuwa nje wakasema, ‘Watu hawa wamejaa mvinyo mpya, wamelewa.’”

¹⁰⁷ Mnaona, tunataka, kumchukua Yesu kuwa Mwokozi wetu, bali si Bwana wetu. Hao waliokuwa wakitenda hivyo si mitume, ilikuwa ni Kristo ndani yao akitenda. Matendo ya Roho Mtakatifu ndani ya mitume. Mitume walikuwa watu kama ulivyo wewe na nilivyo mimi, lakini Roho Mtakatifu aliwafanya watende tofauti, kwa sababu Yeye alikuwa amekuwa Mtawala kamili maishani mwao, hawakuwa na sifa na kiburi tena.

¹⁰⁸ Mwangalieni Nikodemo, alikuja usiku, na kusema, “Bwana, tunajua ya kuwa Wewe ni Mwalimu umetoka kwa Mungu kwa kuwa hakuna mtu awezaye kufanya mambo ufanyayo Wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye.”

¹⁰⁹ Yesu akasema, “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi hata kuuona Ufalme wa Mungu.”

¹¹⁰ Kiburi. Ni kitu gani kilichokuwa kinawazuia Mafarisayo wasimfanye Yeye Bwana? Waliamini Yeye alikuwa ndiye Kristo, bali ilikuwa ni kiburi chao.

¹¹¹ Unasema, “Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa linaloninii. . . .”

¹¹² Sijali, hilo ni sawa, baki katika kanisa hilo, bali acha Yesu awe Bwana moyoni mwako. Acha Yeye awe na mamlaka, si wewe

tena, ni Yeye. Halafu basi, hebu tuondoke kwenye mlango huo, tungeweza kukaa hapo muda mrefu.

113 Lakini hebu twende kwenye mlango mwingine mdogo.

“Loo, kaa mbali na huo!”

114 Ni kitu gani hiki? “Maisha yangu binafsi.” Loo, hutaki mtu yeyote achezee maisha yako ya kibinafsi, akikwambia ya kwamba huwezi kunywa pombe tena, huwezi kuvuta sigara tena, huwezi kwenda kwenye kilabu chako cha wanawake kucheza karata tena. La, hutaki kujipumbaza nacho, lakini nakwambia, Kama ukiwahi kumwacha Yesu awe Bwana wa moyo wako, utaachana nacho, Yeye ataridhisha kila shauku.

115 Unamwonea aibu, unaona aibu kwamba ungea- . . . kwamba unawaletea shutuma watu wako, marafiki zako. Afadhali kila mtu ulimwenguni aniache, bali kamwe usiniache nimletee Yeye shutuma. Acha niishi kwa Neno, Neno la Mungu. “Maisha yangu ya kibinafsi.”

“Sasa, sisi, kila alasiri tunaenda *hivi-na-hivi*.”

116 Na baadhi ya watu hata Wakristo, loo, watu wanaojiita Wakristo, wanaokiri kuwa ni watu watakatifu, wanaanguka mbali sana, hawataki tena utawala wa Kristo.

117 Ninakaa kwenye moteli. Na jana usiku, ng’ambo yake palikuwako na ka—kanisa dogo, na, loo, nilikuwa nimeketi chumbani mwangu, ndipo nikasikia kitu kikilia, nisingeweza kufungua dirisha, kwa sababu hayo madirisha hayafunguki, nikashuka upesi kwa vipandio na kuangalia kote katika nyumba hiyo, nikasema, “Hilo linasikika zuri kwangu.”

118 Nalo kundi la watu limesimama nje uani wakiwacheka wale watu ng’ambo ya barabara katika mkutano mdogo, wakiililia nafsi, wakimwomba Mungu kabisa.

Nikasema, “Inasikika kama Mbinguni kwangu.” Jamani!

119 Hebu Kristo aingie, awe Bwana, huru. “Yeye anayewekwa huru na Mwana yu huru kweli kweli.”

120 Kama umefungwa na hadhi yako ya kijamii, heshima yako ya kijamii. . . Wamarekani wamechafuliwa na sifa za kijamii. Makanisa yenu yamechafuliwa na makusanyiko ya karamu za supu, na michezo ya kamari, na bahati nasibu, na upuuzi makanisani. Baadhi ya wahubiri wakifunga mapema Jumapili asubuhi kusudi wa—washiriki waweze kwenda kuvua samaki au kuwinda. Kuvua samaki na kuwinda ni sawa, bali si lazima kufanywe Jumapili, hiyo ni siku ya Bwana.

121 Watu wengi huachilia makanisa yao mapema kwa ajili ya, nchini mwetu, kwa sababu baa zinafunguliwa saa sita, wanaweza kutumia alasiri kidogo kwa amani. Mtu yeyote anayefanya hivyo amemkosea Mungu.

¹²² Samahani, enyi wasikilizaji, kama nikifanya usumbufu mbaya hapa. Je, lingekuwa ni jambo ovu kwenu, ama, jambo lisilo la kawaida, kumwona nguruwe kwenye kitalu katika lundo la samadi akila? La hashu, hiyo ndiyo tabia yake. Lakini unapomwona mwana-kondoo mahali pale pale pachafu, sasa hilo kweli lingekuwa ni jambo la kuchukiza sana, kwa sababu inaonyesha ya kwamba mwana-kondoo huyo amepotoshwa, alichukua tabia ya nguruwe. Nami ninapomwona Mkristo anayedai kuwa mtumishi wa Mungu. . .

¹²³ Huku nimeketi jana kwenye mkahawa, maskini msichana mmoja alikuja, akasema, “Una uhusiano na kundi lililoko kule linalofanya mkutano huu?”

Nikasema, “Mimi ni Ndugu Branham.”

Akasema, “Ninataka kusema ya kwamba hao watu ambao wamekuwa hapa ndani ndio watu wazuri kuliko wote niliopata kuona.”

¹²⁴ Wakati uo huo, makasisi wawili waliketi pale huku ukosi umepinduliwa upande huo mwingine, nao walikuwa wakinywa mvinyo wa martini na divai. Ndipo walipomalizia chakula chao cha jioni kwa kiko kikubwa, basi mvulana wangu mdogo mwenye umri wa miaka minne, mitano akasema, “Baba, huyo ni mtumishi wa Mungu?” Mtoto mwenye umri wa miaka mitano alijua vinginevyo.

¹²⁵ Sina neno dhidi ya watu hao, huenda wameketi hapa sasa. Ninachomaanisha kusema, ndugu, unasema umeokoka, Biblia ilisema, “Kwa matunda yao mtawatambua.” Si vibaya kwangu kumwona mwenye dhambi hapa nje mtaani, amelewa; si vibaya kwangu kumwona mwenye dhambi akiwa na kiko mdomoni mwake, ama sigara mkononi mwake, si kosa, si—sifikirii chochote kulihusu, yeye ni nguruwe, hajui tofauti. Ninapomsikia mtu akikiri kuwa Mkristo!

¹²⁶ Nilimwambia mmoja, “Mbona, unafanya hivi?”

Akasema, “Hii inaburudisha, hii ndiyo raha yangu.”

¹²⁷ Jinsi ibilisi alivyopotosha hilo! Mungu alimwumba mwanadamu apate kuona kiu, Mungu alimfanya mtu atamani raha, bali alimfanya mtu akiwa na mahali moyoni mwake pa kuonea kiu, na kutamani sana, na kustarehe, na kupata raha, bali raha hiyo ni katika Bwana. Unathubutuje, huna haki yoyote!

Unasema, “Mimi ni raia wa Marekani.”

¹²⁸ Naam, lakini kama wewe ni mwana-kondoo, mwana-kondoo huachilia haki zake. Mwana-kondoo hana ila kitu kimoja, hicho ni sufu, yeye hujilaza chini moja kwa moja, hafanyi vituko hata kidogo, wote hunyolea mbali, ile waliyo nayo.

¹²⁹ Kama wewe ni Mkristo halisi, mwana-kondoo halisi wa Mungu, uko tayari kuachilia haki zako za Kimarekani upate

kuwa Mkristo, maana tabia yako imebadilishwa, Mungu moyoni, Bwana akiwa na mamlaka kamili.

Unasema, “Mbona . . .”

¹³⁰ Watu wanaona aibu kusema, “Amina.” Watu wanaona aibu kumsifu Bwana. Ninaamini ilikuwa ni Finney, Charles G. Finney, sina hakika ilikuwa ni Finney, ninaamini ndiye, aliyekuwa akienda huko nyuma ya chumba chake cha kusomea, ama, ofisini mwake kuomba. Basi siku moja wakati akipiga magoti huko nje, chini ya mti wa kale uliokuwa umeanguka chini, alikuwa akiomba, na wakati akiomba, alifikiri mtu fulani alikuwa anakaribia, ndipo akasimama upesi, akasafisha koo lake, na kusema, “Ahem! Ahem!” Ndipo akasimama na kuangalia pande zote, na hapo Mungu akamsadikisha.

¹³¹ Akasema, “Unanionea aibu, bali ungefikiri lilikuwa ni jambo kubwa kama mtu fulani angekuona ukizungumza na bosi wako. Ungesimama moja kwa moja karibu na bosi wako na kuzungumza, ungewazia ilikuwa ni majaliwa. Uwaache watu wote wa ofisini waone kwamba ulikuwa na majaliwa ya kuzungumza na bosi wako, na Mimi ni Bwana wako na unanionea aibu.”

Akaanguka kifudufudi na kusema, “Bwana Mungu, nisamehe kama mwenye dhambi.”

¹³² Alisema alihubiri jumbe zile zile alizokuwa amehubiri hapo awali, lakini wakati mwingine alipozihubiri, zilivuviwa, zilifanya jambo fulani. Roho Mtakatifu akamshika, akawa mmoja wa wahudumu mashuhuri sana tangu Mtakatifu Paulo. Kwa nini? Alimwacha Mungu aingie na kuchukua mamlaka, akachukua maisha yake ya kibinafsi, kiburi chake kama msomi, chochote alichokuwa. Kama uko tayari kufanya hivyo, kama uko tayari kumwacha Mungu awe na njia huru moyoni mwako!

¹³³ Hebu twende kwenye mlango mwingine kabla hatujaliacha somo hili. Kuna mlango mwingine moyoni unaoitwa, “Imani,” huu ni mlango mkuu. Loo, unamruhusu Yesu aingie kukuokoa, lakini inapofikia kukupa imani uliyopewa na Mungu, unamkataza mlango huo, “Usiuchezee huu, kanisa langu linahubiri siku za miujiza zimepita.”

¹³⁴ Lakini Kristo akiingia kwa mlango huo, haya hapa Maneno atakayosema: “Mimi ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

¹³⁵ Anawathibitishia wale watakaoufungua mlango wa imani, hutachafuliwa na hizo kufuli mlangoni. Acha Kristo asimame mlangoni, Yeye atakwambia ya kwamba Maandiko ni ya kweli.

¹³⁶ Wakati Petro alipohubiri kwenye Siku ya Pentekoste, wakati hao watu walipokuwa wakiyumbayumba chini ya ushawishi wa Roho Mtakatifu, nao ulimwengu wa kidini, watu waliotakaswa, wasomi mashuhuri, na waandishi, madaktari wa torati walisimama nje na kuwacheka watu mia moja na

ishirini wakiyumbayumba na kutenda kana kwamba walikuwa wamelewa, walipoulizwa habari zake, mtume Petro, aliyepewa funguo za Ufalme, walisema, “Tufanye nini tupate kuupokea huu?”

¹³⁷ Akasema, “Tubuni kila mmoja wenu,” akawaambia hao *wanaojiita* waaminio kutubu kutokuamini kwao, “tubuni, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtampokea Roho Mtakatifu, kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu,” na kwa wale walio kwenye Maporomoko ya Klamath, Oregon, “hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie,” ahadi ni kwa ajili yetu.

¹³⁸ Na wakati mtu fulani anapojaribu kufunga mlango huo, na kusema, “Hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya wakati mwingine, Roho Mtakatifu si wa wakati huu,” wanalikana Neno la Mungu aliye hai.

¹³⁹ Lakini wakati Roho Mtakatifu, Kristo, atakapoingia awe Bwana, Yeye atasema, Waebrania 13:8, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele”; atasema, Yohana Mtakatifu 14:7, ama, 8: “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya”; atasema, Marko 16 lilikuwa ndilo agizo la mwisho alilolipa Kanisa, “Enendeni, basi, ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; Asiyeamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: Katika Jina Langu watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya; wakishika nyoka au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.”

¹⁴⁰ Kama Kristo anaweza kuingia moyoni, aingie kwenye mlango wa imani, atakufanya uamini ya kwamba mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio.

¹⁴¹ Mliona Biblia ikinena juu ya kanisa hili katika siku hizi? “Kwa kuwa wasema ya kwamba mimi ni tajiri,” nyakati tajiri sana kanisa limewahi kuwa nazo, wakati wa ufanisi sana kanisa limewahi kuishi ni sasa, majengo makubwa, mahali pazuri, wahudumu wenye elimu, wasomi.

¹⁴² Tuna wahudumu bora kuliko tuliowahi kuwa nao, tuna makanisa bora kuliko tuliowahi kuwa nayo, huku ulimwengu ukizama kila siku katika dhambi. Tuna mimbara dhaifu kuliko tulizowahi kuwa nazo, hiyo ndiyo sababu, watu ambao hawataki kujisalimisha kwa Mungu, hawaninii... Loo, watasema, “Nimeokoka, nimemwacha Yesu aniokoe.” Lakini hutamruhusu kuwa Bwana, asiye akakaa nawe muda mrefu, na hiyo ndiyo sababu unarudi ulimwenguni tena. Hiyo ni kweli kabisa.

¹⁴³ Sasa, ni kitu gani kinachotukia? Katika saa hii tunayoishi, wakati Yesu anapoingia... Angalia kile Yeye alichosema, “Wewe, kwa sababu unasema, ‘Mimi ni tajiri na nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu,’ tuna wachungaji walio bora sana,

wasikilizaji waliovalia vizuri sana, makanisa mazuri sana ambayo kanisa limewahi kujua, sisi. . . “Kwa kuwa wasema ya kwamba mimi ni tajiri na nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu, hujui,” sasa mnaona, wao ni wenye kuungama, wanamwacha Kristo aingie moyoni kuwaokoa, “lakini hawajui ya kuwa wao ni wanyonge, wenye mashaka, uchi, vipofu, wala hawajui.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁴⁴ . . . naye alikuwa kipofu. Nawe unaenda unajaribu kumwambia, “Mama, njoo nyumbani, upesi, una—unajianika, uko uchi.”

¹⁴⁵ Angesema, “Niondokee, ewe mtakatifu anayejibingirisha, ninajua mahali nilipo,” mwanamke huyo ana kasoro fulani kiakili. Yeye yuko hivyo, wala hajui; yeye kweli hajui. Yeye hajifanyi hajui, *hajui*, Biblia ilisema hajui. Yuko uchi, wala hajui. Anajaribu kujifunika kwa majani ya mtini, kama Hawa alivyofanya bustanini, bali kusimama mbele za Mungu, asingeweza. Mwenye mashaka, mnyonge, uchi, kipofu, wala hajui.

¹⁴⁶ Kama mtu angekuwa maskini, mwenye mashaka, mnyonge, kipofu, na uchi, na iwapo alijua hilo, angejaribu kujisaidia. Lakini mtu anapokuwa katika hali kama hiyo, wala hajui, wala hatasikiliza, huwezi kumwambia, hatasikiliza.

¹⁴⁷ “Loo, nasimama mlangoni nabisha.” [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] Huo ndio wakati ambao Yeye angesimama na kubisha. “Kama mtafungua tu na kuniruhusu ningie na kuchukua mamlaka, nitawavika kitani safi.” Loo, haki ya Roho Mtakatifu, “Nitawavika, nitawaondolea aibu yote, nitaweka jina lako katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo, nitakupa Uzima wa Milele.”

¹⁴⁸ Loo, utachukiwa na ulimwengu, bila shaka, “Wote wanaoishi maisha ya kitauwa katika Kristo Yesu,” Biblia inasema, “watateswa. Nitakufanya kile unachopaswa kuwa.”

¹⁴⁹ Basi kumbukeni, Biblia ilisema walikuwa vipofu, vipofu. Loo, kuna vipofu wengi sana siku hizi! Alisema, “Nakushauri uje ununue Dawa ya macho kutoka Kwangu, nipate kuyapaka macho yako upate kuona, Dawa ya macho.” Hiyo Dawa ya macho ni Roho Mtakatifu.

¹⁵⁰ Nililelewa Kentucky, na jamani, tuliishi kwenye kibanda kidogo cha magogo, kilichokuwa, kimejengwa kwa magogo na kukandikwa na matope; na mengi ya hayo yalikuwa yameanguka, kwa sababu kilikuwa cha kale. Nasi tulikuwa na viezeko vya mbao juu ya nyumba, navyo viliwekwa kwenye wakati huo katika mwanga wa mwezi. Navyo hivyo viezeko vilikuwa vimetengana namna *hii*, nayo mvua ingevuma ndani, theluji ingeingia, na kilikuwa tu na vyumba viwili, hakina sakafu ndani yake, udongo mtupu.

¹⁵¹ Nami ninakumbuka Baba alikuwa ametutengenezea sisi wavulana wadogo be—benchi ya kukalia nyuma ya me—meza ya kipande cha mti, kilichokuwa kimekatwa kwa msumeno kutoka kwenye kipande cha gogo huku kimeshikiliwa na vijiti chini yake, na maskini jiko dogo la vipandio mle ndani, Mama alikuwa na kasha la kale lililowekwa juu ya vipande viwili vya go—gogo, lilikuwa na vibonyeo vidogo ndani yake, kabati kuukuu vivyo hivyo, na hivyo, vitanda kadhaa, hivyo tu ndivyo tulivyokuwa navyo.

¹⁵² Na sisi wavulana wadogo ilitubidi kulala darini. Pia kulikuwa na ninii... Walikuwa na nguzo mbili zilizokatwa zikapigiliwa vijiti vidogo, na huko juu, kulikuwako na maskini m—mto wa nyasi kavu, na kwenye mto huu wa nyasi kavu kulikuwa na mto wa manyoya.

¹⁵³ Ndipo Mama angekuja pale usiku na kutufunika mablanketi yote aliyokuwa nayo, na makoti, halafu juu yake angeweka kipande cha turubai, kwa sababu kama mvua ingenyesha, tungeweza kuingia chini ya turubai hii, kama theluji ingeanguka, isiangukie kwenye nyuso zetu.

¹⁵⁴ Na hawa Branham watatu wadogo wamelala kule juu, upepo ukivuma kupitia kwenye viezeko hivyo usiku, labda tungepatwa na baridi, na kushikwa na baridi machoni mwetu. Halafu kesho yake asubuhi, Mama angetuita, angesema, “Billy, shuka uje.”

Nami ningejaribu kufungua macho yangu, nisingeweza kufanya hivyo, ndipo ningempiga ngumi ndugu yangu, Edward, nilimwita Humpy, nikasema, “Unaweza kushuka?”

Akasema, “Macho yangu yameshikamana, pia.”

Ndipo tungempiga Melvin ngumi, tuone kama angeweza kushuka, “La, macho yangu yanashikamana, pia.” Kumbe tumeshikwa na baridi, Mama alitwambia, usiku kucha.

Nami nikasema, “Mama, si—siwezi kushuka chini.”

Akasema, “Kwani kuna nini, Billy?”

Nikasema, “Unajua, macho yangu yamejaa matongotongo.”

¹⁵⁵ Aliyaita matongotongo, sijui ilikuwa ni nini, ilikuwa baridi. Naye akasema, “Macho yako yamejaa matongotongo.” Akasema, “Vema, ngojeni tu kidogo, Mpenzi.”

¹⁵⁶ Sasa, mama ya—yangu ni nusu-Mhindi, baba yake alikuwa mmoja wa wawindaji hodari sana niliopata kuwajua. Basi alikuwa akiwinda, naye angewatega rakuni hawa na kuwauza. Na, mwajua, wakati angewapata hao kuuni, wangekuwa wanene, na kwa hiyo angeminya mafuta, basi mafuta ya kuuni yalikuwa ndiyo tibu-yote nyumbani mwetu, hiyo tu ndiyo dawa tuliyokuwa nayo huko nyuma kabisa.

¹⁵⁷ Sijui ni wangapi waliowahi, hapa, waliowahi kuketi karibu na mshumaa wa grisi, kipande kidogo cha uzi katika... Hakika.

Ni wangapi wamewahi kuchoma fundo la msonobari wapate . . . ? Vema, hivyo ndivyo ilivyotubidi kufanya jambo hilo.

¹⁵⁸ Ndipo moto wa jirani ulipozimika, tungechukua moto kutoka mekoni mwetu wenyewe, tukaenda kule kusaidia kutengeneza . . . Hamna miti ya kiberiti wala chochote kile, iliwabidi kuuwasha kwa kipande cha jiwe gumu, ama kitu fulani, kupashana moto. Nami ninakumbuka ya kwamba walikuwa wakifanya hivyo mara nyingi, nyingi sana kwa sepetu, na kushuka barabarani kwenda kwa jirani. Na wakati . . . Tulikuwa na maisha magumu siku hizo.

¹⁵⁹ Halafu basi, ninakumbuka Mama angesema, “Hebu kidogo, mpenzi.” Naye angeninii . . . Tungeshikwa na kifaduro. Mnajua angefanya nini? Angechukua kijiko kilichojaa mafuta haya ya kuuni, na—na kuyamwagia tapentaini, halafu akayanyunyizia sukari kidogo, ilitubidi kuyameza hayo. Sijui hilo lilifanyia nini koo linalouma, lakini, vyovyote iwavyo, tulipona, Mungu ni Mungu mwenye rehema.

¹⁶⁰ Ndipo wakati macho yetu yote yangeshikamana, angesema, “Hebu kidogo, Mpenzi.” Naye angewekelea kopo la kale la mafuta ya kuuni juu ya stovu, naye angechemsha vizuri yapate joto, naye huyo angepanda vipandio, ngazi fupi tu ya kale, akapanda pale na kuyasugua macho yetu kwa mafuta hayo ya kuuni mpaka yakafunguka.

¹⁶¹ Vema, hiyo itakuwa sawa kwa jicho la kawaida, lakini ninawaambia, kumekuwa na hali ya hewa baridi sana ikipitia kanisani. Hiyo ni kweli. Nao wana kufungwa kwa macho ya kiroho, nako kutahitaji zaidi ya mafuta ya kuuni kuyafungua, itabidi nguvu za Roho Mtakatifu kuingia machoni mwao.

¹⁶² “Shauriana Nami, njoo ununue Dawa ya macho kutoka Kwangu, ninapobisha mlangoni. Hebu niingie na kuyafungua macho yenu, niwapake Dawa ya macho machoni mwenu, itayafungua macho yenu.”

¹⁶³ Hujui . . . Kama Elisha, pamoja na, huko chini Dothani pamoja na mtumishi wake, wakati lile—lile jeshi, wale wageni, walipokuja na kuuzingira mji wote wa Dothani, naye akasema, huyo mtumishi akaamka, naye akasema, “Baba yangu, jeshi lote la Shamu liko juu yetu!”

¹⁶⁴ Naye yule nabii wa kale, mwajua, angeweza *kuona*, kwa hiyo akasimama, akaangalia kote, akasema, “Naam, hiyo ni kweli, bali kuna wengi walio pamoja nasi kuliko walio pamoja nao.”

Naye akasema, “Sioni mtu yeyote ila wewe.”

¹⁶⁵ Ndipo akampaka Dawa ya macho, akanyosha mkono na kushika kichwa chake, akasema, “Bwana, yafumbue macho ya mvulana huyu apate kuona.” Ndipo macho yake ya kiroho yalipomjia, Malaika wa Moto walikuwa wamemzunguka nabii

huyo, na magari ya Moto, na milima inayowaka Moto. Mnaona, yeye alikuwa kipofu, wala hakujua.

¹⁶⁶ Wapo watu wengi leo ambao ni vipofu, wala hawajui wema wa Bwana, watu waaminifu, wanyofu wasiojua wema. Huelewi jinsi Mungu alivyo mwema, ni raha jinsi gani kumtumikia, ni ra—raha jinsi gani.

¹⁶⁷ Siku moja sina budi kusimama, siku moja nitafunga Biblia yangu kwa mara ya mwisho, sina budi kukutana na Mungu na nikatoe hesabu kwa ajili ya kila mmoja wenu. Na kila mtu kuninii. . . Nadhani nimehubiri moja kwa moja ama kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa watu milioni ishirini ama thelathini kote ulimwenguni, kuzunguka mara saba, na ni—ni—ninajua sina budi kuwajibika kwa jambo hilo. Nami sina budi kuwa katika uaminifu mkamilifu, na kujua ya kwamba ninawaambia ukweli.

¹⁶⁸ Hamtambui wema wa Mungu. Laiti mtu, mwenye dhambi, angeweza tu kuyafungua macho yao na kuona jinsi Mungu alivyo mwema! Laiti Yeye angaliweza kusugua Dawa kidogo machoni mwao, ndipo waweze kuangalia kote na kuona jinsi alivyo mwema!

¹⁶⁹ Huko chini Shreveport, Louisiana, si muda mrefu uliopita, kulikuwako na. . . Nilikuwa huko chini nikihubiri katika mkutano wa hema. Nilikuwa nimemfuata Billy Graham huko nje kwenye u—uwanja wa besiboli. Na—na kulikuwako na ndugu mzee, mweusi kule chini, naye alikuwa mhubiri mzee mashuhuri, mwenye roho nzuri, naye alikuwa na mzee mmoja kanisani mwake jina lake, jina lake lilikuwa Gabriel, lakini kwa namna fulani tulimwita Gabe, kifupi.

¹⁷⁰ Na, lakini kamwe asingeliweza kujiambatanisha na kanisa, angeenda kanisani, naye alikuwa na mwanamke mzuri, mtauwa, mtakatifu. Nao wakamwomba Gabe, nao wakafanya yote waliyoweza kumfanya Gabe aende kanisani na kutenda mema, bali asingefanya hivyo.

¹⁷¹ Ila alipenda kwenda kuwinda, basi siku moja yeye na mchungaji walikuwa huko nje wakiwinda, ilikuwa ni Jumamosi moja alasiri, na mzee Gabe alikuwa hana shabaha, asingeweza kupiga chochote. Lakini alipokuwa akija alasiri hiyo, yeye na mchungaji walikuwa tu wamelemewa na wanyama wote walioweza kuwabeba, ndege, na sungura, na kuchakulo. Nao walikuwa wakija kwenye njia ya kale waliyoiuia ambayo walikuwa wamesafiria mara nyingi, basi jua la Jumamosi alasiri lilikuwa linatua magharibi.

¹⁷² Naye mchungaji, akiongoza njia ameshika bunduki yake mabegani mwake, na wote wawili wamebeba mawindo, wakitembea pale, naye akaona alipoangalia nyuma, Gabe aliendelea kuangalia nyuma juu ya bega lake kuelekea machweo

ya jua. Mchungaji hakushtushwa sana na jambo hilo, kwa hiyo akaendelea mbele tu.

¹⁷³ Ndipo baada ya kitambo kidogo, mkono mweusi mkubwa mno, ukawekwa begani mwake, naye akageuka kumwangu Gabe. Basi machozi yalikuwa yakitiririka tu kutoka kwenye mashavu yake makubwa, meusi, naye akasema, “Mchungaji, kesho asubuhi *mimi taketi* pamoja na mke wangu mpendwa mbele ya kanisa, nami ninawatakeni mnibatize katika ubatizo wa Kikristo, na hapo nitabaki mpaka Yesu atakaponiita nyumbani.” Akageuka na kuangalia upande wa jua tena.

¹⁷⁴ Akasema, “Gabe, unajua ninathamini hilo.” Kasema, “Nataka kukuuliza jambo fulani.” Akasema, “Ni mahubiri gani niliyohubiri yaliyokufanya ugeuke, ama kwaya iliimba wimbo gani uliokufanya ugeuke, na kufanya uamuzi huu kwa ajili ya Kristo?”

¹⁷⁵ Akasema, “Mchungaji, *ninathamini* kila mahubiri uliyowahi kunihubiria. *Ninathamini* kila ombi ambalo watakatifu waliwahi kuniomba, na nyimbo ambazo kwaya iliimba, lakini,” kasema, “unajua, hilo silo lililosababisha jambo hilo.” Kasema, “Niliangalia nyuma kwenye jua lile, nami nikatambua jua langu linatua, pia.”

¹⁷⁶ Akasema, “Ndipo nikaangalia, huku wamening’inia kote mwilini mwangu, hao wanyama.” Akasema, “Unajua, siwezi kupiga chochote risasi,” kisha kasema, “hata hivyo, leo hii Yeye amenipa wanyama hawa wote, wa kutosha kudumu juma lote lijalo.” Akasema, “Hakika, Yeye ananipenda, la sivyo asingekuwa mwema hivi kwangu.”

¹⁷⁷ Akasema, “Nilimsikia akibisha moyoni mwangu, nami nikageuka ulipokuwa ukiendelea mbele, nami nikaufungua moyo wangu na kusema, ‘Karibu, Bwana Yesu, ukachukue nafasi Yako moyoni mwangu.’” Kisha kasema, “Akafanya hivyo, Yeye sasa ni Bwana wangu tangu wakati huu na kuendelea.”

¹⁷⁸ Loo, laiti tungaliangalia nyuma ya mabega yetu na kuona jinsi Mungu amekuwa mwema kwetu, kuona tu wema Wake kwa mwenye dhambi, kuona ya kwamba amekuleta salama umbali huu! Ukiketi ukiwa na akili timamu, angalia nyuma, ni Nani aliyekulisha? Ni nani aliyekuvisha nguo? Wakati breki hizo zilipokuwa zikipiga kelele na gari nusura likugonge, ni Nani aliyekulinda wakati huo? Alikuwa ni nani Huyu katika saa hiyo ya ugonjwa wakati daktari alipotikisa kichwa chake, kasema, “Sijui lolote zaidi la kufanya.” Lakini uko hapa usiku wa leo, angalia nyuma kidogo uone kilichotukia.

¹⁷⁹ Kwako wewe Mkristo, hebu angalia tu kote na uone ulimwengu wenye dhambi, jinsi ulivyo, na kujua ya kwamba Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alikuchagua kwa uteuzi, na kuweka jina lako kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo, na kubisha moyoni mwako. [Ndugu

Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] Nawe ukaufungua na kumruhusu aingie. Jinsi Yeye alivyo mwema!

¹⁸⁰ “Tazama, nasimama mlangoni nabisha, na kama utafungua mlango, nitaingia kwako, nami nitakula pamoja nawe, kula pamoja naye, naye pamoja Nami.” *Kula* maana yake ni, “kuburudisha, ku—kuwa na ushirika.” Kula mmoja na mwenzake, ni kufanya ushirika, kushirikiana.

¹⁸¹ Unaweza kuufungua moyo wako, kila mlango, na kusema, “Bwana, ingia ndani. Usiwe tu Mwokozi wangu, bali uwe Bwana wangu, Mtawala wangu, Kiongozi wangu, nichukue jinsi nilivyo. ‘Jinsi nilivyo tu bila ombi moja, lakini kwamba Damu Yako ilimwagwa kwa ajili yangu.’ Jinsi tu nilivyo, Bwana, nitakuamini Wewe?”

¹⁸² Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi. Kabla tu ya kuomba, sijui kama kungekuwa na mtu hapa ambaye humjui Bwana Yesu kama Mwokozi wako, nawe ungetaka tu kuinua mkono wako, na kusema, “Kweli, Mhubiri, ni kweli kwamba si—si—simjui, kamwe sijamwacha awe Bwana wangu.”

¹⁸³ Labda umemkubali Yeye kama Bwana wako, lakini kamwe huwezi wala hutaki kuyasalimisha maisha yako yote Kwake, usalimishe kila kitu ulicho nacho Kwake. Ufungue kila mlango na umkaribishe tu, na useme, “Bwana Yesu, ni—nitakuruhusu uingie kwa moyo wangu wote. Wewe uchukue mnara wangu wa utawala, Nawe unidhibiti tangu sasa.”

¹⁸⁴ Hivi mngetaka tu kuinua mikono yenu, na kusema, “Bwana, nikumbuke”? Mungu akubariki, mtoto mdogo. Je, kungekuwa na...? Mungu akubariki, bwana. Je, kungekuwako na wengine zaidi, ungeinua tu mkono wako, useme, “Mungu, chukua mamlaka makamilifu”? Mungu akubariki, ewe msichana. Mungu akubariki, ndugu. Hilo ni zuri sana.

¹⁸⁵ Kila mtu aombe tu sasa: “Bwana, yatie macho yangu mafuta usiku wa leo. Labda nimekuwa mtoto mpumbavu. Kama mauti yangekuja chumbani mwangu usiku wa leo, nami ningeagizia, upesi, daktari aitwe, naye angekuja kule, aseme, ‘Ni mshtuko wa moyo. Kijana mwanamume, kijana mwanamke, mzee, hakuna kitu ninachoweza kukufanyia, kuna donge la damu lililokwama moyoni,’” unahisi mishipa ikipoa mikononi mwako, ikipanda mkononi mwako, nawe uko karibu kufa, huku wewe unaondoka, loo, jinsi unavyotaka Yeye achukue mamlaka kamili wakati huo. Lakini kwa nini isiwe sasa? Itakuwa imechelewa sana wakati huo.

¹⁸⁶ Labda, kama mngeinua tu mikono yenu, ingemaanisha mengi sana usiku wa leo. Mungu akubariki, ewe msichana. Huenda kukawa na mwingine? Mungu akubariki, huko nyuma.

¹⁸⁷ Hatukuombi ujiunge na kanisa, wewe nenda kwenye kanisa lolote unalotaka, tunakuomba tu umruhusu Yesu awe na

mamlaka kamili. Mungu hataniuliza Siku hiyo ni kanisa gani nililowaongoza watu kuendea. Siwaongozi kanisani, ninawaongoza kwa Yesu. Njoo, acha Yeye aingie. Utafanya hivyo?

¹⁸⁸ Haitachukua muda mrefu, labda umelala hapa kando ya barabara katika ajali kesho, kesho yake, mwezi mmoja kuanzia sasa, miaka kumi kuanzia sasa, damu ikitiririka kutoka kwenye mishipa yako, nawe unajua ni mapambano mengine machache tu nawe umekwisha, ukigaagaa katika damu yako mwenyewe.

¹⁸⁹ Kijana katika upeo wa ujana wako, katika uzuri tu wa maisha, mbona, “Mkumbuke Muumba wako siku za ujana wako,” kwa nini usiunie mkono wako kumkubali sasa? Siku moja, utazeeka kama ukiishi. Haitachukua ila masaa machache tu. Wewe tu ni... Unakomaa tu kuanzia umri wa miaka kumi na mitano hadi ishirini, ndivyo sayansi isemavyo, kisha unaanza kufa baada ya hapo.

¹⁹⁰ Msichana mrembo, wa kupendeza, ni Nani aliyekuumba hivyo? Kwa nini uliumbwa hivyo? Si kwa ajili ya malisho ya kuzimu, dada mpendwa, bali kwa ajili ya Ufalme na sifa za Mungu. Hivi hutalitambua sasa? Maskini uso huo wako wa kupendeza, mtu huyo mdogo, mrembo uliye wewe, haitachukua muda mrefu mpaka nywele hizo zitakapokuwa zinaingia mvi, mabega hayo yataungana, taabu za maisha katika miaka michache ijayo zitakudhoofisha. Huenda ukamhuzunisha na kumwondoa moyoni mwako kwa mara ya mwisho. Kumbuka, anapobisha, mruhusu aingie.

¹⁹¹ Waweza kuinua mkono wako, useme, “Nikumbuke, Mchungaji, niombee,” kabla hatujaomba? Mungu akubariki, mama. Hilo ni zuri sana. Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki. Hilo ni zuri. Mungu akubariki.

Mtu mwingine angesema, “Nikumbuke, ndugu, na—na—nataka ninii... Mungu aje moyoni mwangu. Ni—ni—ni...”

¹⁹² Ndilo jambo muhimu sana linaloweza kutukia. Kumbuka, maisha yaliyo marefu sana ni ya miaka sabini tu, lakini Umilele ni wa kudumu, kwa kuwa Umilele, hauna mwanzo wala mwisho. *Daima* ni kipindi tu cha wakati; *Milele* inaendelea na kuendelea, dahari na dahari za wakati bado itaendelea mbele.

¹⁹³ Je, wewe...? Ni Wakristo wangapi humu ndani ambao kamwe hawajamfungulia Kristo mioyo yenu yote kumwacha Yeye awe Mtawala, Bwana, na Mungu? Kama ungetaka Yeye afanye hivyo, na unamtaka afanye hivyo maishani mwako, maisha yale uliyobakiza, huenda wewe ni kijana, huenda kuna watu wengi walioketi hapa wenye umri wa miaka sabini watakaoishi zaidi ya mvulana ama msichana mwenye umri wa miaka kumi na mitano, kumi na sita, kama ukiishi mpaka asubuhi, utaishi zaidi ya mamia yao, inua mkono wako, na useme, “Mungu, unirehemu. Bwana, chukua mamlaka kamili juu

ya moyo wangu, chukua yote niliyo mimi, nakupa wewe, jinsi tu nilivyo.” Waweza kuinua mkono wako?

¹⁹⁴ Mungu akubariki, ewe Mkristo, wewe Mkristo, wewe, wewe, naam, jamani, kote, kila mahali. Utajisikia tofauti unapoinua mkono wako, inaonyesha ya kwamba kitu fulani... Ukimtetea Kristo hapa, Yeye atakutetea Kule; kama ukimwonea aibu hapa, Yeye atakuonea aibu Kule. Hivi hutampokea sasa? Nashangaa, wakati tukiimba huu kwa upole sana:

Jinsi tu nilivyo, bila hata ombi moja,
Lakini kwamba Damu Yako ilimwagwa kwa
ajili yangu,

¹⁹⁵ Mbona...? Sijui kama ninyi mliokuwa mmeinua mikono yenu, nanyi ambao hamkuinua, mnetaka kufanya ninii... Mkristo angetaka kuja pamoja na mwenye dhambi usiku wa leo. Mwenye dhambi anakuja kwa sababu anatambua ya kwamba Mungu ameyaokoa maisha yake, na kumweka nje ya kuzimu muda huu wote; Wakristo huja ambao wanajua na kuthamini ya kwamba Mungu amekuwa mwema sana kwake kuyaokoa maisha yake, mwanamume au mwanamke.

¹⁹⁶ Sijui, usiku wa leo, kama haungekuwa wakati mzuri kwetu kuja madhabahuni na kufanya maombi ya kujiweka wakfu, papa hapa sasa kanisani. Kweni ninyi washiriki wa kanisa, kila mmoja wenu, hebu tuje madhabahuni tunapoimba, hivi mtakuja?

Jinsi tu nilivyo, bila hata ombi moja,
Lakini kwamba ninii Yako...

¹⁹⁷ Njoo, rafiki mwenye dhambi, waliorudi nyuma, mfuasi wa kanisa, Mkristo.

...mimi,
Na kwamba Wewe umeniamuru nje Kwako,
Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, naja! Naja!
Jinsi tu nilivyo, Wewe utanipokea,
Utakaniribisha, utanisamehe, utanitakasa,
utanipokea;
Kwa sababu ninaahidi ninaamini,
Ee Mwana-Kondoo wa Mungu, naja! Naja!

¹⁹⁸ Mwenye dhambi, njoo, Mkristo, njoo, onyesha shukrani zako, chukua msimamo kwa ajili ya Mungu, njoo tu moja kwa moja huku. Kama unataka Yesu aingie moyoni mwako, fungua kila mlango, mpe njia huru, njoo.

¹⁹⁹ Hapa siku moja, wengi wenu mmesikia hadithi hiyo, wakati watu wanakusanyika, Danny Greenfield, yeye alikuwa mwinjilisti mashuhuri, alivuka... alipitia Oregon hapa, yapata miaka hamsini iliyopita, akavuka Marekani, usiku mmoja aliota ndoto kwamba alikufa. Ninawatakeni mnisikilize. Alidhani

alikuwa katika ndoto yake, kama anavyoisimulia katika kitabu chake, naye alisema alipanda juu kwenye malango ya Mbinguni.

Naye akasema huko juu kwenye lango la Mbinguni, mlinzi wa lango alisema, “Ni nani anayepakaribia Mahali hapa Patakatifu?”

²⁰⁰ Naye akasema, “Mimi ni Danny Greenfield, mwinjilisti wa Kimarekani. Ninakikaribia Kiti cha Enzi cha neema cha Mungu, ninatamani kuingia na kuchukua Nyumba yangu ya Mbinguni.”

Akasema, “Hebu kidogo, Bw. Greenfield, hebu nione kama jina lako liko kwenye Kitabu.”

Ndipo akarudi, akasema, “Samahani, bwana, jina lako haliko kwenye Kitabu.”

Akasema, “Loo, hakika, umekosea!”

Akasema, “Nina kila jina, wala hakuna jina katika Kitabu hiki.”

Akasema, “Nifanyeje? Nilikuwa mwinjilisti.”

Akasema, “Kuna jambo moja tu ninalojua kwako kufanya, ni kusimama kwenye Kiti cha Hukumu.”

²⁰¹ Vema, hilo tu ndilo alilopaswa kufanya, hakukuwa na uamuzi mwingine wa kufanywa. Alisema alianza kusogea, akawazia, katika ndoto yake, kupitia angani, naye akaanza kuingia kwenye Nuru, akaanza kupunguza mwendo, polepole zaidi na zaidi kadiri Nuru ilivyokuwa ikiongezeka zaidi. Hatimaye, nuru ikawa nyingi sana hata ilikuwa vigumu kwake kuona chochote, ndipo akasimama, akasema alisikia Sauti kuu. Basi niliposoma hayo, moyo wangu ulitetemeka. Mwinjilisti huyo mashuhuri!

²⁰² Naye alisema ya kwamba alisikia Sauti ikisema, “Ni nani anayekaribia kiti Changu cha haki?”

²⁰³ Akasema, “Mimi, Baba, Danny Greenfield, mwinjilisti wa Kimarekani.” Akasema, “Nilikuja kwenye malango ya huu Mji, nami nikafukuzwa, na ilinibidi kukata rufani mbele ya haki Yako.” Akasema, “Ninasimama katika kivuli cha haki yako, Bwana. Hivi kuna rehema yoyote kwa ajili yangu?”

²⁰⁴ Yeye akasema, “Basi nitakuhukumu kwa sheria Yangu.” Rafiki, kamwe usingojee kufika kwenye Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi, afadhali upate rehema sasa. Basi akasema, “Nitakuhukumu kwa sheria Zangu.” Akasema, “Danny Greenfield, uliwahi kusema uongo maishani mwako mwote?”

²⁰⁵ Akasema, “Nilifikiri nilikuwa ni mwaminifu na nilikuwa nimesema kweli. Lakini,” kasema, “Mbele ya ile Nuru kuu, niliona nilikuwa nimewaambia mambo ambayo hayakuwa sawa kabisa.” Akasema, “La, ni—nilidanganya.”

Akasema, “Basi, Danny Greenfield, uliwahi kuiba?”

206 Naye akasema, “Kama kuna chochote nilidhania nilikuwa, kilikuwa ni mwaminifu. Lakini,” kasema, “Mbele ya Nuru hiyo, niliona biashara nyingi ndogondogo nilizofanya ambazo hazikuwa sawa kabisa.”

207 Ndugu, huenda usiwazie hilo sana usiku wa leo, dada, lakini Mbele ya Nuru hiyo, utawazia mambo mengi sana wakati huo, haitakuwa kama ilivyo sasa.

208 Naye akasema, “Danny Greenfield,” baada ya kunukuu Amri, akasema, “Je, umekuwa mkamilifu? Haki yangu inahitaji ukamilifu.”

209 Akasema, “La, Bwana, sikuwa mkamilifu.” Kisha kasema, “Nilikuwa nikisikilizia nisikie mlipuko huo mkubwa: ‘Ondoka Kwangu, ewe mtenda maovu, uende kwenye maangamizi ya milele, yaliyowekwa tayari kwa ajili ya ibilisi na malaika zake.’”

210 Kisha kasema, “Papo hapo, wakati mifupa yangu ilionekana kana kwamba ilikuwa imetenguka,” kasema, “Nilisikia Sauti tamu kuliko zote niliyowahi kusikia,” kasema, “Nikageuka kuangalia, nami nikaona uso wa kupendeza kuliko zote niliowahi kuona.” Kasema, “Hakuna sauti ya mama wala uso wa mama ungeweza kuwa wa kupendeza kama uso huo.” Kisha kasema, “Alikuwa karibu nami, akanikumbatia kwa mikono Yake.”

211 Akasema, “Baba, ni kweli kwamba Danny Greenfield hakuwa mkamilifu duniani, lakini wakati alipokuwa kule, alifanya jambo moja: Alinitetea wakati alipokuwa kule. Na sasa nitamtetea Hapa, na hatia yake yote iwekwe juu Yangu.”

212 Nashangaa usiku wa leo, ndugu, dada, kama ungeweza kuwa na mtu mwingine yeyote, mchungaji, ama rafiki, ama kanisa, ama chochote kingeweza kukusimamia, mbali na Damu ya Bwana Yesu. . . Hivi hutamtetea usiku wa leo, kusudi apate kukutetea siku ile? Ukitaka, unakaribishwa uje ujiweke wakfu kwa Bwana huku tukiimba mara nyingine tena.

Jinsi tu. . .

213 Mtete. Yesu alisema, “Ukinionea Mimi aibu hapa, nitakuonea aibu Kule.” Njoni sasa, sivyo? Chukueni msimamo. Jiwekeni wakfu, ewe Mkristo, yaweke wakfu upya maisha yako. Simameni moja kwa moja kwenye marefu ya kanisa, mkitaka. Kama hakuna nafasi katika marefu ya kanisa, simameni moja kwa moja kwa miguu yenu, papo hapo mlipo, simameni kwa miguu yenu.

. . . ahadi naamini,
Ee Mwana-kondoo wa Mungu, naja! Naja!
. . . bila kungojea

Sikiliza huu:

Kuondolea nafsi yangu ninii moja . . . (Moja tu,
hiyo ndiyo inayohitajika kukuhukumu.)
Kwako Wewe, ambaye Damu Yako inaweza
kusafisha kila doa,
Ee Mwana-kondoo wa Mungu, naja! Naja!

214 Na tuinamishe vichwa vyetu sasa. Kila mmoja, kwa njia yako mwenyewe, jinsi unavyoomba kanisani mwako . . . Wenye dhambi wanaosimama, kama tu vile mwenye dhambi katika Biblia angeweza tu kujipiga mwenyewe kifuani, na kusema, “Bwana, unirehemu mimi, mwenye dhambi.” Alienda nyumbani amehesabiwa haki. Usiogope, ewe mwenye dhambi, utafanya vivyo hivyo usiku wa leo, kama utafanya tu maombi ya mwenye dhambi, “Unirehemu, Ee Mungu.”

215 Kweni ninyi Wakristo, mpeni ibada ya moyo wenu, sifa. Jiji hili, tangu nimekuwa hapa, naona ya kwamba linahitaji uamsho. Uamsho si kuingiza wafuasi wapya, bali kuamsha kile ulicho nacho. Sasa, kuna wahudumu wengi wanaosimama, kuna watu watakatifu wanaosimama kumshukuru Mungu, kuna wenye dhambi wamesimama, waliorudi nyuma, washiriki wa kanisa wamesimama.

216 Sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu, kumbukeni, Yeye amebisha moyoni mwako. “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu.” Mnajua hilo? Vipi kama ulikuwa mtu huyo ambaye Mungu kamwe hakusema naye? Vipi kama ulikusudiwa maangamizi ya Milele kama Farao alivyokuwa, kama Pilato alivyokuwa? Mungu kamwe asingeweza kuugusa moyo wako.

217 Si muda mrefu uliopita huko chini Tennessee, katika kanisa la Kibaptisti, niliongozwa kumwendea msichana mmoja nyuma ya kanisa, alikuwa binti wa shemasi, nami nikamwuliza, nikasema, “Bwana anahusika na wewe, sivyo, dada?”

Akasema, “Kama ningetaka mtu fulani anizungumzie namna hiyo, ningetafuta mtu aliye na akili.”

218 Nikatoka nje ya jengo, kichaka cha waridi kilikuwa kimesimama pale, nilipokaribia, loo, jinsi mwanamke huyo alivyonizungumzia kijeuri! Msichana mdogo anayevutia sana.

219 Yapata miaka miwili baadaye, nilipitia mahali pale, naye huyo hapo alikuwa akishuka kwenda mtaani. Mama aliyekuwa na tabia nzuri, mavazi yake ya ndani yakining’inia chini, alionekana mchafu, akivuta sigara. Ndipo nikawazia huyo alikuwa ni yule msichana, nami nikavuka barabara, nikashuka upande ule mwingine, kidogo nyuma yake.

220 Alijua ya kwamba mtu fulani alikuwa akimfuata, akapunguza mwendo. Alipokaribia, alisema, “Halo, Mhubiri.” Loo, jamani! Basi akasema, “Unanikumbuka?”

Nikasema, “Naam, mama, ninakukumbuka.”

Akaingiza mkono kwenye pochini yake, akasema, “Karibu sigara.”

Nikasema, “Jionee aibu!”

Akasema, “Labda ungekunywa pombe?”

Nami nikasema, “Hili halijatendeka, sivyo?”

Akasema, “Hivi utaingia nyumbani kwangu hapa? Ninataka kuzungumza nawe.”

Nikasema, “Hivi hungeweza kuzungumzia hapa mlangoni?”

Basi akasema, “Unakumbuka usiku ule ulipotoa wito wa madhabahuni?”

Nami nikasema, “Naam, mama, hakika ninakumbuka.”

²²¹ Kasema, “Ninataka kukwambia jambo fulani, hiyo ilikuwa ndiyo nafasi yangu ya mwisho.” Akasema, “Nilimhuzunisha mara nyingi kupita kiasi.” Akasema, “Bw. Branham,” akasema, “moyo wangu umekuwa mgumu sana tangu wakati huo...” Sasa sikilizeni tamshi hili, nilimwuliza kama ningeweza kulinukuu, naye akasema ningeweza. Akasema, “Moyo wangu umekuwa mgumu sana, mpaka ningeweza kuiona nafsi ya mama yangu ikikaangiwa kuzimuni kama chapati maji, na kuicheka.” Hiyo ni kwa ajili ya kumkataa.

Usimkatae, usimkatae...

Yesu...?...moyo wako kuongoza,

Ingawa umepotea.

Loo, jinsi utakavyotamani Yeye aseme,

“Umefanya vema,”

Kwenye ile Siku ya Milele!

Usimkatae Mwokozi mpendwa moyoni

mwako,

Usimkatae.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

²²² Baba yetu wa Mbinguni, Injili ya kale ya thamani, ingawa imeteswa na kukokotwa kupitia kila namna ya mahali penye giza, lakini hata hivyo inaangaza kuliko chochote ulimwengu umewahi kutoa, utakaso kwa ajili ya nafsi, zeri katika Gileadi kwa ajili ya wasio safi. Tuna furaha sana kwamba Damu ya Yesu Kristo katika siku hii, ambapo wakati tukijua ya kwamba taifa letu karibuni litalipuliwa vipande-vipande, kulingana na unabii wa Biblia...

²²³ Haitachukua muda mrefu, Bwana, tutakapoona bunduki na silaha za atomiki ambazo zimetundikwa katika kila taifa, zikingojea tu moja ipitie kwenye skrini ya rada, ndipo ulimwengu mzima utaingia... Wanasayansi tayari wamesema ni chini ya dakika tatu kabla ya usiku wa manane. Ambapo watu wa ulimwengu wa kisayansi wanalionga, mara nyingi, kabla ya wale wanaojita Wakristo kuweza kulitambua!

224 Mtu huyo mashuhuri, hivi majuzi, alisema kama angeiweka kwenye redio au televisheni, sayansi yetu maarufu sana katika taifa hili ilisema ya kwamba watu wangeingia kichaa barabarani wakipiga mayowe wapate rehema. Mungu, na kuwazia kabla hilo halijatukia, Wewe uliahidi ungekuja kwa ajili ya Kanisa Lako. Kuja Kwako kumekaribia jinsi gani, Baba?

225 Tunasimama hapa, usiku wa leo, katika vivuli vya rehema Yako. Ninakuletea Wewe kusanyiko hili, Bwana. Nimewapa Injili, kwa kweli nijuavyo mimi kutoka katika Biblia, kwamba Wewe unasimama katika wakati huu wa Laodikia, ambapo watu wanajihesabia haki kwa kuwa mfuasi wa kanisa ama kukariri kanuni fulani ya imani, na hata hivyo hawatakaribisha Wewe kama Bwana moyoni mwao. Nilifanya vizuri nijuavyo, Baba, kwa uongozi wa Roho Mtakatifu.

226 Kwa kweli mamia wamesimama kwa miguu yao. Ninaomba, Bwana Mungu, ya kwamba kila Mkristo hapa atayaweka maisha yake wakfu upya Kwako, sasa hivi. Bwana Mungu, jalia mwenye dhambi ajisalimishe kikamilifu, afungue kila mlango, kila njia wanayopaswa kuishia, na Kristo asimame kwenye kichwa cha nyumba, kichwa cha mlango, kichwa cha nafsi yao, akili yao, na kutenda kupitia kwao apate kufanya mapenzi Yake. Tujalie, Bwana.

227 Mbariki kila mmoja hapa. Wabariki wagonjwa na wanaoteseka. Jalia wale wanaosimama sasa ambao hata ni wagonjwa, jalia ya kwamba Roho mkuu wa Mungu aponyaye atatenda kazi juu ya jengo hili. Mponye kila mgonjwa aliyesimama hapa. Tujalie, Bwana.

228 Mwokoe kila mwenye dhambi, na umjaze kila mwaminio, na umtie moyo kila Mkristo asonge mbele. Tujalie, Bwana. Tunakutolea Wewe ibada ya moyo wetu, tunakusifu kwa yote yaliyo ndani yetu, tunainua mioyo yetu, tunainua mikono yetu, tunainua sauti zetu, tunainua yote tuliyo, Bwana, katika Uwepo Wako, tupokee, Ee Bwana. Tunajiweka wakfu sasa Kwako. Chukua kanisa hili kuu, lililokombolewa la Mungu aliye hai, litakase, Baba, lijaze na Roho Mtakatifu.

229 Roho wa Mungu na aenee juu ya jengo hili sasa, awaleweshe watu. Ee Mungu, wape furaha ya Bwana, wapate kujazwa na Roho Mtakatifu kama walivyokuwa kwenye Siku ya Pentekoste, ili kwamba tangu saa hii na kuendelea, nguvu za Mungu zitasonga mbele, zifikie kila kanisa na kila mtu, wapate kujazwa na wema wa Mungu, ili nguvu za Mungu ziweze kutenda kazi kupitia kila mtu, na kila nafsi ibarikiwe.

230 Jalia watu wawe mitaani kesho, wakishuhudia, wakimtukuza Mungu, wanaume na wanawake kazini mwao, wakimpa Mungu sifa. Saa imewadia, Bwana, ambapo tunakutazamia kuja Kwako wakati wowote. Hebu tusimame na

nyuso zenye aibu, jalia tujazwe na wema Wako na Roho Wako. Tujalie, Bwana, tunapokuomba maombi yetu yenye bidii.

²³¹ Katika Jina la Yesu Kristo, tunakupa kusanyiko hili. Ninajitoa Kwako, niliyatoa maisha yangu Kwako miaka thelathini na mmoja iliyopita, Bwana, Ee Mungu, nisaidie kuishi kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Nisaidie, Bwana, kuwaongoza watu Kwako, kuingia katika Uwepo huo uliobarikiwa wa tumaini hilo la Milele linalokaa, Ng'ambo ya pili. Ee Mungu, tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili. Nafsi zetu zimesuguliwa, roho zetu zinajisikia safi, tumejiweka wakfu Kwako.

²³² Baba Mtakatifu, utuweke katikati ya mapenzi Yako, tukizitenda amri Zako, tukizifuata amri za Mungu, tukichukua amri za Mungu na kuishi kwazo. Tujalie, Bwana. Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo na ikae juu yetu daima, kwa rehema za Mungu tunasihi, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²³³ Ni wangapi wenu ninyi Wakristo usiku wa leo wanaopenda ninii...? Kuhubiriwa kwa Neno ni kama tu, vema, ni kama nusikaputi inayokufanya ulale kwa ajili ya upasuaji, ili kwamba Mungu aweze kuondoa mambo ya ulimwengu kutoka kwako, nusikaputi ya Roho Mtakatifu anapokupulizia, nawe unalala, ndipo Tabibu mkuu anaanza kufanya upasuaji kwa kisu Chake, na kuyakatilia mbali mambo ya ulimwengu.

²³⁴ Ni wangapi wanaojisikia ya kwamba kwa kuwa umesimama kwa miguu yako na kuyaweka maisha yako wakfu kwa Mungu, kwamba unajisikia kama mtu tofauti? Inueni mikono yenu namna hii. Mungu ashukuriwe.

²³⁵ Hebu na tumwimbie Yeye ule wimbo mzuri wa kale wa kanisa, sisi sote pamoja basi:

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kalvari.

Vema, kila mtu pamoja sasa, sote pamoja:

Na...

Na tuinue mikono yetu tunapouimba.

...nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Na...

Imbeni tu kwa moyo wenu sasa. Ujumbe umekwisha, abuduni tu katika Roho.

...mpenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu

Mtini Kalvari.

²³⁶ Sasa, tunapouvumisha, ninataka upeane mikono na mtu aliye karibu nawe, na kusema, “Salamu, Mkristo, rafiki msafiri.” Peaneni mikono ninyi kwa ninyi, msemi, “Mungu akubariki.” Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Pentekoste, Nazarayo, Pilgrim Holiness, chochote mliche, peaneni mikono.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu

Mtini Kalvari.

²³⁷ Sasa hebu na tuinue mikono yetu, na kumwambia Mungu huku macho yetu yamefumbwa, kwa sauti kubwa tuwezavyo sasa, kwa sifa Zake. Mwimbieni sasa:

Na . . . , nampenda
Kwani Yeye . . .

Mpungie mkono wako.

. . . alinipenda
Na kununua ninii yangu . . . 

60-0711 Mlango Ndani Ya Mlango
Shule Ya Sekondari Ya Juu Ya Klamath Union
Klamath Falls, Oregon Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org